<sup>11</sup> Evi vinu-vi vyanukwambire-vi, amuru, na ufunde. <sup>12</sup> Usimwase awaonse kufezeyi unemba wako. Ila ka wenye kwamini, uwé nfano mwema, kati ya namuna yako yakusowera, yakuinshi, yakupenda, yakuntumaini Mwenyezimungu, na ya uswafi wako. <sup>13</sup> Mpaka omi nije, vinu-vi shugulikira: kufyoma baina Mandiko, kuwarimbisa myoyo wenye kwamini, na kuwafunda. <sup>14</sup> Usase uwezo maalumu wawisusiriwe. Kumbukira kuwa uwezo-wu kupewa julu ya kubushuriwa pawakuturire makono wakulungwa wa jamati. <sup>15</sup> Vyanukwandikire-vi tunza sana-sana, vinu-vi ufulate. Kwa javyo, kukula kwako kolotiwa baina ka wanu piya. <sup>16</sup> Risunge sana mwaneyewe na usunge vyauri kufunda. Zidi kushugulikira novyo. Ukitenda javyo, urivusha uwe pamoja na wanu wari kukusikira-wo.

## 5

*Namuna za kuinshi na wenziwo wenye kwamini*

<sup>1</sup> Nukutafadali nkulungwa usimwinyukire, ila unrimbise moyo kamba wawayo. Wanemba uwarimbise myoyo kamba wanduzo, <sup>2</sup> wanawaka wakulungwa uwarimbise myoyo kamba wamamazo, na wári uwarimbise myoyo kamba walumbuzo, kwa uswafi piya.

*Manankweli na jamati*

<sup>3</sup> Kuhusu manankweli, wenshimu ware sawana munu mwengine wakuwasaidiya. <sup>4</sup> Fala nankweli mojawapo akiwa nawo wana au ujukulu, ewo wajuzi wanze kutenda ibada na jamaa pakaya pawo, maripo akuwaludisira makolo, kamana eci ndi kinu cema cakusakikana mbere ya Mwenyezimungu.

<sup>5</sup> Basi, nankweli wakweli, saana munu mwengine wakunsunga, iye tamaa yake katula ka Mwenyezimungu. Iye ázidi kulebela na kutenda duwa usiku na nsana. <sup>6</sup> Fala nankweli ainshi vimwajibu iye mwananyewe, ingawa kawa hai, nkati ya roho kafwa. <sup>7</sup> Na kuhusu ezi shuruti-zi, wamuru, ipate manankweli na jamaa zawo wasisutumiwe na wenziwawo.

<sup>8</sup> Munu akitowa kuntafiti jamaa yake, kuzidi pakulu pakaya pake, iye kankukatala kwamini kwetu, basi kawapunda wanu sawamini.

<sup>9</sup> Nankweli andikiwe nkati ya kipinga cakusaidiwa na jamati akiwa munu wa hirimu ya myaka sitini au zaida, akiwa muka âlombiwe na nlume mmoja tu basi\*, <sup>10</sup> akiwa munu alavyanga ushahidi julu ya vitendo vyema-vyema, akiwa munu awarerire wanawe, akiwa munu akolotanga wema ka wayeni, akiwa munu awatumikiranga wenziwe wenye kwamini ka kurinyenyekeya, akiwa munu awasaidiyanga wenye uzuni, na akiwa munu akishugulikiranga piya vitendo vyema.

<sup>11</sup> Kuhusu manankweli wári, uwakatare nkundi-mo, kamana pawasaka kwasa njira ya Almasihi, viwajibu kulombiwa tena upya. <sup>12</sup> Wakilombiwa tena upya, wakuja kuhukumiwa kwa kuwa kwamini kakwanza wasa. <sup>13</sup> Kuno warifunda ufuko, wapita-pita manyumba. Visitoshe wakuwa watesi na ware wazuda, wakisowera vinu savijuzi kusoweriwa. <sup>14</sup> Basi, kuhusu manankweli wári-wa, vinajibu walombiwe tena upya, wawapongore wana wawo, wamiliki sana pakaya pawo. Kweli, wasimpe mbishani wetu wakutilaumu anta nafasi mmoja. <sup>15</sup> Wamojawapo wazungunuka futi, wankunfulata Ibilisi.

<sup>16</sup> Akiwapo mwanamuka mmojawapo njamati ari na jamaa nankweli, ansunge, awe amiri wa nankweli-yo. Iye aajuzi kuremeresa jamati ipate jamati-yi iwasunge manankweli wakweli.

*Inshima ka wakulungwa*

<sup>17</sup> Wakulungwa walongoza jamati sana wajuzi wasifiwe pakulu pawenye, kuzidi watenda juhudi ya kwereza na kufunda. <sup>18</sup> Kwa faida yawo, Mandiko akwamba:

“Ng'ombe asáya mafuluwela,  
kanywa yake usinfunge.”

Na Mandiko akwamba novyo tena:

“Nshahara waapokéra nkolakazi, únjuzi.”

<sup>19</sup> Nkulungwa mmojawapo wa jamati, ukisikira kalongoperiwa kinu, usikubali, sazi-lawirire kanywa za mashahidi wawiri au watatu. <sup>20</sup> Wakóla dambi, uwasutumumu mbere ya wenye kwamini piya ipate wope wengine-wo novyo.

<sup>21</sup> Nankukulaizirani mbere ya Mwenyezimungu na Almasihi Insa pamoja na malaika watondoriwe kuwa fulata vyanukutuma-vi, usinang'anize kumaso, usimpendeleye

\* 5:9 Au: “ákiwa mwaminifu ka nlumake”.

munu. <sup>22</sup> Pausaka kuntula makono kuntawaza munu awe nlongozi, usitende upesi-upesi. Ukitenda javyo, uringiza madambi ake. Madambi a wanu wengine usiringize, rikengere uwé swafi.

<sup>23</sup> Usinywe tena maji matupu, ila na vinyu neyo tumira aba, kwa sababu ya ntumbokulu rako na malwazo ako mara nyingi zawenye†.

<sup>24</sup> Kuhusu wanu wamojawapo, madambi awo awoneka baina sawanalamuriwa suku ya Kiyama. Ila kuhusu wengine, madambi awo awafulata, aawoneka mpaka suku ya Kiyama. <sup>25</sup> Novyo-novyoni, kábula Kiyama víwoneka baina vitendo vyema-vyema. Anta savyanzire kuwoneka, mwinsho avifisika tena.

## 6

<sup>1</sup> Wari sini ya nzigo wa utwana, mamwenye wawo wawature kuwa ndi wenye kujuzi kwishimiwa nfululu ipate zina ra Mwenyezimungu na kufunda kwetu visikufuririwe.

<sup>2</sup> Na ware wari na mamwenye wenye kwamini, wasiwafezeyi kwa kuwa nkati ya kwamini munu na nduye. Wajuzi wawatumike pakulu sana kwa kuwa ndi wenye kwamini wakuwapenda, ware wapokerera faida ya kazi yawo.

### *Inlimu za ulongo na mali a kweli*

Vinu-vi wafunde na warimbise myoyo. <sup>3</sup> Wanu wamojawapo wafunda inlimu nyengine yakusiyana, awakubali usemi mwema wa Mwenye wetu Insa Almasihi, na awakubali kufunda vyaifulata ibada. <sup>4</sup> Nowa wanu-wa kuwéjala kuridāi, awereriwa na kinu anta kimoja. Kweli, ewo walwere wa kukaidi, na kuhusu mana a masemo, watendanga ushinda. Vinu-vyo visalamula wiyana, umani, kufuru, dana mbaya sapano shariya, <sup>5</sup> pamoja na kukaidiyana sakuna mwinsho. Piya-vyo visalamuriwa na wanu wakupombonyoriwa ankili, wakukosa ukweli, wadaniza kuwa ibada namuna ya kupata faida ya mali.

<sup>6</sup> Kweli-kwelini, iwapo faida ulu ka munu wa ibada akitenda na radi. <sup>7</sup> Atijire mulumwengu-mu na kinu, na tikifwa, atisukula anta kinu. <sup>8</sup> Basi, tiwe radi, tikiwa nawo cakurya na nguwo. <sup>9</sup> Fala wanu wa kuwajibu utajiri wagwirira kushetwaniwa, kukoreka nnambo na wájibu mwingi sauna mana na waajali. Vitendo-vyo viwazamisa wanu mpaka kuwa dhiki na kuwaribu. <sup>10</sup> Kweli, wájibu wa nzuruku ndi nzipe wa ubaya piya. Nzuruku-wu, wamojawapo, kwa kuwajibu pakulu wapate mwingi, wasika, wasa kwamini, warisoma na malwazo mengi awenye.

### *Kulaiza ka mwinsho*

<sup>11</sup> Uwe, mwananlume wa Mwenyezimungu, evyo vinu-vyo, tira! Fulata shariya na tenda ibada, fulata kwamini pamoja na pendo, fulata kuhitamili pamoja na wororo.

<sup>12</sup> Utende ushinda, ushinda mwema wa kwamini. Korera mainsha a milele kwa kuwa ndi cawitiriwe. Kuhusu noya, kulavya ushahidi mwema mbere ya mashahidi wengi.

<sup>13</sup> Mbere ya Mwenyezimungu, Mwenyé mainsha ka viyumbe piya, na mbere ya Almasihi Insa (noyo Insa-yo kálavya ushahidi mwema mbere ya Pontiyu Pilatu), <sup>14</sup> mbere yawo, nankukwamuru javi: fulata ezi shuruti-zi bila baka wala kulaumiwa, mpaka kuludi ka Mwenye wetu, Insa Almasihi. <sup>15</sup> Mwenyezimungu anludisa wakati wake watondore:

Iye ndi Mwenyezimungu ntukufu,

mmoja tu basi Mwenyé Uwezo,

Nfalume wa mafalume,

Mwenye wa mamwenye.

<sup>16</sup> Mmoja tu basi saafwa milele,

ainshi nnuru saiwandikika.

Aapo ammonire manziro, aapo akidiri kummona.

Mwenyé utukufu, Mwenyé mamulaka milele! Aamina.

<sup>17</sup> Matajiri wa sambu-wa, wamuru wasiridāi wala wasitumaini nzuruku saukawa kulainika. Ila wawajuzi kuntumaini ndi Mwenyezimungu atipa piya vinu kwa wingi tivuze. <sup>18</sup> Wamuru watende vyema, wawe matajiri wa vitendo vyema. Wasiwe wa coyo,

† 5:23 Dalili maji-yo aari swafi.

wawe tayari kuwamera wengine. <sup>19</sup> Wariturire aliserusu ngema mbere ipate wakupate mainsha a kweli.

<sup>20</sup> He, Timotiyu, amana-yo riturire. Usowezi wa makafiri saufã, risapuse. Usowezi wakukaidiyana witiwa wawijiwifu sauri, risapuse. <sup>21</sup> Wamojawapo kwa kuwa wafulata nowo usowezi-wo, kwamini wabonya.

Neema iwe pamoja namwe!

## Waraka 2 ya Paulu ka Timotiyu

### Mwanzo

Eyi ndi waraka ya mwinsho yaandike Paulu myaka 64-68 bandi ya Almasihi. Iye kandika ari nkalaboshu mojawapo ya Roma, akirindira kuulaiwa. Ingawa akiwona javi mwinsho wa uhai wake, mwinsho wa kazi yake, pamoja na kukosa ka wengi nkati ya marafiki zake (kwa sababu ya wofi wa kulumbatiwa), iye ákizidi kuntaya nguvu Timotiyu kuhusu kutejemera katiri nawo ka Almasihi. Akisowera kuhusu faida ya mafunzo swafi, atiri nawo mmandiko, na faida iripo ya kuwafunda wenye kwamini wapya.

### *Salamu*

<sup>1</sup> Omi Paulu, walii wa Almasihi Insa kamba vyaasaka Mwenyezimungu, niperekiwe kwereza tamaa ya mainsha atiri nawo kwa kulungana na Almasihi Insa. <sup>2</sup> Nukwandikira uwe Timotiyu, mwanangu wanukupenda.

Mwenyezimungu Baba, pamoja na Mwenye wetu, Almasihi Insa, wakujanliye rehema na salama na wakutendere huruma.

### *Kukengera uswafi wa Habari Ngema*

<sup>3</sup> Mwenyezimungu wanintumikanga na moyo saunisusuka kamba vyawakintukuza wababu zangu, noyo ndi waninshukuru. Ninshukuru panukukumbukira ponse panitenda duwa usiku na nsana. <sup>4</sup> Panikumbukira masozi ako, nukuwa na hamu yakukuwona tena inijare radi.

<sup>5</sup> Nikumbukira kwamini kwako ka ukweli, kanzire wiwiyo Loisi pamoja na mamayo Unisi, na mpaka sambipa nanawo uhakika kuwa uwe novyo kwanawo. <sup>6</sup> Ntamana, uwezo maalumu waakwisusire Mwenyezimungu panukukurire makono, nukukumbusa urimbise nowo uwezo-wo. <sup>7</sup> Kamana roho yaatipere Mwenyezimungu aititaya wofi, ila ititaya uwezo, pendo, pamoja na nguvu zakuritunza ofwe wanyewe.

<sup>8</sup> Kwa javyo, usiwonere haya kulavya ushahidi wa Mwenye wetu, wala kuhusu omi nfungwa wake, ila kutabika pamoja nami kwa Habari Ngema, na uwezo wa Mwenyezimungu. <sup>9</sup> Mwenyezimungu ndi ativushire na ndi atitondore tiwe umati wake-wakeni. Eci siyo kwa sababu ya vitendo vyetu, ila kwa kupanga iye mwananyewe, na rehema yake yaatipewe tangu milele julu ya Almasihi Insa. <sup>10</sup> Rehema-yo tifafanuririwa epa sambijulu ya kulawirira Nvushi wetu, Almasihi Insa. Iye kafuja kifo, na visitoshe, julu ya Habari Ngema, kafafanula baina mainsha a milele. <sup>11</sup> Kwa kwereza na kufunda noyi Habari Ngema-yi, omi nitondoriwa niwe mwerezi na walii na mwanlimu, <sup>12</sup> ndimana nankutabika novyo. Fala siwona haya, konta nimwijiwa ire waniri kuntumaini, na nanawo hakika kuwa iye kanawo uwezo wakusunga sana vire vyaanigabizire omi, mpaka suku ya Kiyama.

<sup>13</sup> Vyaunisikire omi, tula kamba nfano wa inlimu yakweli, ka kuzidi kwamini na kwa pendo ratiri nawo kwa kuwa tilungana na Almasihi Insa. <sup>14</sup> Na julu ya Roho Takatifu ári nkati yetu ofwe, sunga ankiba ngema vyaugabiziwe.

<sup>15</sup> Kamba vyawijiwa, piya wanu wa Aziya wanitipuka. Munkonjo mwawo, kawapo Figelo na Heromogeni. <sup>16</sup> Ila Oneziforu anirimbisanga moyo mara nyingi, na aawona haya ingawa omi niwa nfungwa. Mwenye Insa awolotere huruma iye na jamaa zake. <sup>17</sup> Iye paafikire Roma, katenda juhudi mpaka kaniwona. <sup>18</sup> Mwenye Insa amwase Oneziforu-yo atenderiwe huruma na Mola suku ya Kiyama-yo. Ukwijiwa sana-sana namuna vyaanitimike Efezu.

<sup>1</sup> Kwa javyo, uwe mwanangu, rimba moyo julu ya rehema ya Almasihi Insa. <sup>2</sup> Na vinu vyausikire julu yangu omi mbere ya mashahidi wengi wawenye, novyo wagabizi wanu wakamilifu wari nawo uwezo wakuwafunda wanu wengine.

<sup>3</sup> Tabika pamoja nofwe kamba surudadu mwema wa Almasihi Insa. <sup>4</sup> Atumika kuwa surudadu aashugulikira na hali ya eya mainsha-ya, ipate vimwajibu ire antondore. <sup>5</sup> Na novyo, ikiwa munu kankutenda mashindano na mwenziwe, aatuziwa saafulate shuruti za mashindano. <sup>6</sup> Na mwenye kukola kazi yakurima ajuzi awe ntanzi kupata faida ya kazi yake. <sup>7</sup> Eleriwa canamba, kamana Mwenye Insa akupa werevu wa vinu piya.

<sup>8</sup> Kumbukira Insa Almasihi! Iye kafufuriwa ka wafwi, na akiwa ujukulu wa Daudi. Javi ndi vyanereze Habari Ngema yangu omi. <sup>9</sup> Kwa noyo Habari-yo ndi iri kunitabisha, nifungiwa na unyolo kamba kisomi. Fala usemi wa Mwenyezimungu aufungiwe. <sup>10</sup> Ndimana, kwa faida ya ware watondoriwe nihitamili vinu piya, ipate wapate kuvushiwa nkati ya Almasihi Insa pamoja na utukufu wa milele.

<sup>11</sup> Wakwaminika ndi usemi wamba:  
“Tikifwa na Insa, tiinshi naye novyo.

<sup>12</sup> Tikihitamili naye, titawala naye novyo, tikinkana, naye novyo atikana.

<sup>13</sup> Tikintula minyongo, iye azidi kuwa mwaminifu, kamana aakidiri kurikana mwanyewe.”

#### *Mukazi wakwajibisa ka Mwenyezimungu*

<sup>14</sup> Evi vinu-vi, wenye kwamini wari pamoja nawe, wakumbuse. Na mbere ya Mwenyezimungu, wamuru kuwa wase kukaidiyana kuhusu masemo, konta akuna faida, kuwaribu wenye kusikira. <sup>15</sup> Sakula kuroloa mbere ya Mwenyezimungu kamba munu wakwajibisa, ntumisi sariwonera haya na kazi yake, wakufunda sana-sana habari za ukweli. <sup>16</sup> Fala rinyemese kukaidiyana sakuna mana, sakumwinshimu Mwenyezimungu, konta ukuja kuwalongoza wanu kwasa kumwinshimu tena pakulu. <sup>17</sup> Visitoshe, kusowera kwawo kukwenera kamba vyawenera ulwere wa kuulaya. Nfano wake ndi kamba vyawakunishie Himenayo na Fileto. <sup>18</sup> Ewo wasa kufulata njira yakweli, wankupita wakereza kuwa wafwi wesa futi kufufuriwa, wakwangaisha kwamini ka wanu wamojawapo. <sup>19</sup> Fala aliserusu ya ukweli wa Mwenyezimungu ibaki yoloke. Neyo yandikiwa alama javi: “Mola awejiwa wake.” Na yandikiwa tena javi: “Piya wenye kwamba kuwa wawa upande wa Mwenye watire nfululu ubaya.”

<sup>20</sup> Nnyumba mwa tajiri, aviwapo vyombo vya oru na vya parata tu basi, fala vikuwepo vyengine novyo vya mbawo au vya utope. Vyengine viinshimiwa, vyengine aviinshimiwa. <sup>21</sup> Basi, munu akiriswafi vinu vya ubaya vyanisowere-vi, akuwa kamba combo cakuinshimiwa, akiwa swafi, akuwa tayari kutumiriwa na Mwenye kwa piya kazi zake ngema-ngema.

<sup>22</sup> Ritanuse vinu vya unemba vyakuwa, aurikengera, vyakutenza wajibu mbaya. Ila uwe, pamoja na piya wenye kunlebeli Mwenye Insa na moyo swafi, sakula shariya, kwamini, pendo, pamoja na salama. <sup>23</sup> Ritanuse mambo a kukaidiyana kijinga na saana mana, ukijiwa kuwa mwinsho akumanisa. <sup>24</sup> Ntumisi wa Mwenye Insa aajuzi kupita akitenda umani, ila ajuzi olote wema ka wanu piya, awe na uwezo wakufunda vyema, na olote imani. <sup>25</sup> Ajuzi afunde kwa namuna yakurinyekeya ka ware wankatala. Dalili Mwenyezimungu awapindula watubiye, na awapa wijiwifu wa ukweli, <sup>26</sup> waludi wawaze sana, wapolonyoke nnambo ya Ibilisi iwafungire tangu mida ipate watende caasaka iye.

### 3

#### *Tafauti za suku za mwinsho*

<sup>1</sup> Epa sambu, ijiwa kuwa suku za mwinsho, zikuja kulawirira tafauti nyingi zawenye. <sup>2</sup> Kamana wanu wakuja kuripenda wanyewe, wapenda nzuruku, waridai, wawakejeli wenzawo, wakufuru, awawasikiriza wawa zawo, awashukuru, na watafiti vitakatifu kwa namuna mbaya. <sup>3</sup> Ezo suku za mwinsho-zo, wanu awapendana anta na jamaa zawo

newo, na awaswamiiyana. Wawalongopera wenziwawo vinu vya ulongo, awaritunza wanyewe, wakakatima, na wakimiyana na meema. <sup>4</sup> Ewo wawazungunuka wenziwawo, watenda kinu sawawazire sana, waridāi pakulu, na viwajibu vinu vya mulumwengu-mu pakulu koliko Mwenyezimungu. <sup>5</sup> Tena, wanu wa ezo suku za mwinsho-zo, waritula kamba wanu wa dini, fala wakatala uwezo wa dini yakweli. Wanu kamba ewo, wasapuke. <sup>6</sup> Kamana nkati ya ewo ndi ware waringiza mmanyumba, wawatesa wanawaka wa myoyo myepepe. Wanawaka kamba ewo watabishiwa na madambi, wamilikiwa na wājibu mbaya, <sup>7</sup> na daima wafundiwa fala anta suku moja auwerera ukweli. <sup>8</sup> Wanlimu wawafunda nowo wanawaka-wo wabishane na ukweli, kamba wanu wakwitiwa Yane na Yambere\* vyawabishane na Musa. Ankili zawo zaribika, na kwamini kwawo siko ka ukweli. <sup>9</sup> Fala nowo wanlimu-wo awendeleya suku nyingi konta wanu piya wakuja kwijiwa uzozo wawo, kamba vyaviwakunire Yane pamoja na Yambere.

*Paulu vyaanlaizira Timotiyu awe kamilifu*

<sup>10</sup> Sambu, uwe kifulata sana-sana kufunda kwangu, vitendo vyangu, anzima yangu, kwamini kwangu, kuvumirira kwangu, pendo rangu, kuhitamili kwangu, <sup>11</sup> kulumbatiwa kwangu, pamoja na kutabika kwangu kunipatire inti za Antiyokiya, Ikoniyu, na Lishitera. Nilumbatiwa pakulu, fala Mwenye Insa kaninusuru mmakono mwa piya-wo. <sup>12</sup> Ndi kweli kuwa piya wasaka kunfulata Almasihi Insa kamba vyaasaka Mwenyezimungu, ewo wakuja kulumbatiwa. <sup>13</sup> Ila wabaya na walongo wakwendeleya kutenda ubaya, wawatesa wenziwawo, newo wanyewe watesiwa novyo.

<sup>14</sup> Fala uwe, zidi kutenda vyaufundiwe na vyawakikishiwe, ukiwejiwa ware waku-fundire, <sup>15</sup> na ukijiwa kuwa, tangu uri ntoto, kurifunda Mandiko Matakatifu, akupa uwezo wakupata fahamu mpaka uvushiwe, julu ya kuntumaini Almasihi Insa. <sup>16</sup> Mandiko piya alawa ka Mwenyezimungu. Piya afāi atifunda ukweli, atolotera vitendo vya makosa nkati ya mainsha etu, atiduma, na atifunda njira ya ukamilifu. <sup>17</sup> Kwa javyo, nfulati wa Mwenyezimungu akamilike, awe na uwezo wakutenda piya vitendo vyema.

4

*Paulu vyaanlaizira Timotiyu atimize kazi yake*

<sup>1</sup> Sambu, nukutafadali pakulu, mbere ya Mwenyezimungu na mbere ya Almasihi Insa ája kuwalamula wanu hai na wafwi, na kwa sababu ya kuludi kwake kuja kutawala awe nfulume. <sup>2</sup> Nukutafadali wereze usemi wa Mwenyezimungu. Uwe tayari, kuwapo nafasi au kutowa kuwapo. Wadume, wasutumumu, na warimbise myoyo wanu kwa kuwafunda sana-sana na imani. <sup>3</sup> Konta ukuja kufika wakati wanu wawatowa kuhitamili kusikira inlimu yakweli. Ewo wakuja kifulata viwajibu ewo wanyewe, na wakuja kuwasakula wanlimu wakuwafunda viwajibu kusikira ewo. <sup>4</sup> Wakuja kukatala ukweli, wafulata masemo saana mana.

<sup>5</sup> Fala uwe, kwa kila hali, tunza cema na kibaya, tabika vya ubaya, kola kazi uwereze Habari Ngema, na timiza cewo cako.

<sup>6</sup> Kamana mainsha angu amiminika futi. Wakati wangu wakwasa duniya uwa karibu. <sup>7</sup> Nitenda ushinda mwema, nifika mwinsho wa mashindano a kutuwa, nibaki nikamini. <sup>8</sup> Epa sambu, nitengezeriwa lemba ra shariya, nituririwa na Mwenye Insa, mwenyé kulamula shariya suku ulu ya Kiyama. Na aanituriro omi tu basi, fala áwaturira piya wanu warindira na radi kuludi kwake.

*Paulu alaizira vyakumusu Timotiyu*

<sup>9</sup> Tafadali rimbise uje kwangu kuno upesi. <sup>10</sup> Kamana Dema, nakupenda vinu vya mulumwengu-mu, kanitipuka, kalawa koka Tesalonika. Kresike koka Galata, Titu koka Dalmatiya. <sup>11</sup> Ila kuno Luka tu basi ndi abakire nomi. Paulawa kuja kuno, uje na Maruku, konta nkati ya kazi yangu, anisaidiya pakulu. <sup>12</sup> Tikiku nimpereka Efezu. <sup>13</sup> Pauja-po,

\* 3:8 Yane na Yambere wákiwa minabii walongo vibekibeki; ewo watenda maajuza a ulongo mbere ya Musa na Firyaua.

nisukurire kapa rangu ranasire Karupu kaya ya Torowa. Usukure novyo vitabu, kuzidi pakulu vyanandike mmasambala\*.

<sup>14</sup> Alishandere urivi kanitenda vibaya futi. Mwenye amhukumu kwa vitendo vyaa-tendire. <sup>15</sup> More-more naye, konta kabishana na vyatimwambire piya.

<sup>16</sup> Mara yakwanza yakuwa nirikotola yeka, aawerepo anta munu mmoja wakuni-saidiya, piya wanitipuka. Mwenyelimungu awaswamii! <sup>17</sup> Falakini Mwenye Insa ákiwa upande wangu, kanipa nguvu ipate niwereze Habari Ngema wanu Sawari-Mayahudi, piya wasikire. Níkiwa kamba niri nkanywa mwa simba, fala iye kanivusha. <sup>18</sup> Mwenye akuja kunivusha kwa vitendo vibaya piya, na anisukula sana-sana muufalume wake mbinguni. Iye atukuziwe daima milele! Aamina.

*Salamu*

<sup>19</sup> Pisisila na Akila pamoja na wari kuinshi nyumba ya Oneziforu, salamu zawo. <sup>20</sup> Erashitu kabaki Korintiyu, na Torofimu nimwasa Miletu nlwere. <sup>21</sup> Ririmise uje kuno upesi, sainamba kufika mirongo ya baridi. Eubulu, Pude, Linu, Kalaudiya, pamoja na wafulati wa Insa piya, wakuperekera salamu.

<sup>22</sup> Mwenye awe pamoja nowe. Rehema iwe pamoja namwe.

---

\* 4:13 Paulu kandika mmasambala a manyama. Nozo “waraka-zo” zikirimba kupatikana, na zikikala myaka mingi konta zikirimba.



## Waraka ya Paulu ka Titu

### Mwanzo

Paulu kamwandikira eyi waraka-yi Titu kwa ajili ya kumpa nguvu paakitabika na wabishani wake makafiri na wengine njamati wakifunda kuwa ikisakikana kutimiza shariya wapate kwakikishiwa. Na tena Paulu kampa Titu ngano kuhusu namuna ya wanu wakijuzi kutondoriwa kuwa wakulungwa wa jamati, na namuna wenye kwamini vyawakijuzi kuinshi munu na mwenziwe na wengine wari panja ya jamati.

### *Salamu*

<sup>1</sup> Omi Paulu, ntumisi wa Mwenyezimungu na walii wa Insa Almasihi ipate niwasaidiye wanu watondoriwe na Mwenyezimungu wantumaini iye, wejiwe nfululu ukweli vyaisaka ibada. <sup>2</sup> Ukweli-wu ukuja na kurindira mainsha a milele, alavire tamaa Mwenyezimungu tangu mida, na Mwenyezimungu aalongopa. <sup>3</sup> Paufikire wakati maalumu, usemi wake ufafanuriwa julu ya kwereza kwangu kanigabiziwe na Mwenyezimungu Nvushi wetu paanitumire.

<sup>4</sup> Nukwandikira eyi waraka-yi uwe Titu, mwanangu wakweli nkati ya kwamini kwetu kumoja noko.

Mwenyezimungu Baba wetu na Insa Almasihi, Nvushi wetu, wakujanliye rehema na salama.

### *Namuna yakuwatondola wakulungwa wa jamati\**

<sup>5</sup> Omi nûkwasa kisirwa ca Kereta ipate umarize kazi zibakire noko, na uwature walongozi wa jamati kila kaya. Kumbukira vyanukutumire: <sup>6</sup> Nlongozi wa jamati ájuzi ainshi saasutumiwa na shariya, awe nlume wa muka mmoja tu basi, na wanawe wawe wenye kwamini, wasitowe inshima, na wasikire cawambiriwa. <sup>7</sup> Isakikana nkulungwa wa walongozi wa jamati ainshi saasutumiwa na shariya, kwa kuwa alongoza kazi ya Mwenyezimungu. Ntamana, asiwe munu wakuridāi, wala asiwe munu wakwangupa kukimiwa, wala asiwe nrevi, wala asiwe mmani, wala asiwe munu wakumwajibu kutumira nzuruku kwa caputu. <sup>8</sup> Ila noyo nkulungwa-yo ájuzi awapokerere wayeni sana-sana, awe munu wakumwajibu piya vyema, aritunze, awe kamilifu, takatifu, na aridume mwananyewe. <sup>9</sup> Ajuzi oloke na usemi kamilifu waafundiwe, ipate awarimbise wanu julu ya inlimu yakweli, na ware wabísha ukweli, awasutumu.

<sup>10</sup> Kusema kweli, wawapo wengi wabísha, kuzidi pakulu nkati ya “nkonjo wa kupendeleya itani”. Wakwereza vinu savina mana, na wawatenvya wenziwawo. <sup>11</sup> Ewo wajuzi wanyamaziwe, kwa kuwa wawadanganya jamaa piya, wafunda vinu savijuzi kufunda. Anzima yawo ndi kupata nzuruku, anta iwe kwa namuna za aibu! <sup>12</sup> Mpaka mmoja wawo, nabii wa Kereta, kaamba javi:

“WaKereta daima walongo,  
wawa kamba wanyamangalo wakofya.

Ewo wafuko, wawaza kurya tu basi.”

<sup>13</sup> Ewu ushahidi-wu ndi wakweli. Kwa javyo, wasutumu kanguvu ipate wawe nkati ya kwamini ka ukweli, <sup>14</sup> newo wase kusikiriza masemo akubuniwa na Mayahudi, na wase novyo ámuri za ware waturire minyongo ukweli. <sup>15</sup> Piya vinu swafi ka wanu wari swafi, fala ka wabaya na ware sawantumaini Mwenyezimungu, acipo swafi. Anta mawazo awo na fahamu zawo haramu. <sup>16</sup> Nowo wanlimu walongo-wo wakwamba kuwa wamwijiwa Mwenyezimungu, fala vitendo vyawo vikolota kuwa awamwijiwa. Ewo wabaya nfululu, awasikiriza, na awakidiri kutenda kitendo cema anta kimoja.

\* 1:4 Ona 1 Timotiyu 3:1-7.

## 2

*Kufunda inlimu yakweli*

<sup>1</sup> Fala uwe Titu, wafunde namuna yakifulata inlimu yakweli. <sup>2</sup> Wafunde wakulungwa waridume wanyewe, wainshimike, waritunze wanyewe, wakomare kati ya kwamini kwawo, na riwejare pendo na kuhitamili.

<sup>3</sup> Wafunde novyo waka wakulungwa wanshugulikire Mwenyezimungu. Wasipite wakiwasowerera wenziwawo caputu, wala wasiwe watwana wa kirevi. Ila, wafunde namuna ngema, <sup>4</sup> wawafunde wanawaka wári kuwapenda walume wawo pamoja na wana wawo, <sup>5</sup> waritunze wanyewe, wawe swafi, watafiti pakaya, wawe na moyo mwema, na wawatwii walume wawo. Kwa javyo, awatenza aibu usemi wa Mwenyezimungu.

<sup>6</sup> Namuna moja noyo, walange wanemba wainshi wakiritunza wanyewe.

<sup>7</sup> Uwe mwananyewe, kwa piya-vyo, uwé nfanu mbere yawo julu ya vitendo vyema. Na paufunda, tenda bila kudanzira na vyakwinshimika, <sup>8</sup> nakutumira usemi wakweli ipate asiwepo wakukusutumumu. Basi, munu asaka kukukaidi onse awona haya, aawa nawo kinu kibaya cakwamba kwetu ofwe.

<sup>9</sup> Wambire watwana wenendere piya cawambiriwa na mamwenye wawo, na wawa-tendere juhudi viwajibu. Usiwajibu usowezi wakunyata, <sup>10</sup> wala wasiwewire. Kwasa javyo, warolote kuwa wanu wakwaminika ka ukweli kwa vinu piya, ipate inlimu ya Mwenyezimungu, Nvushi wetu, inshimiwe pakulu.

<sup>11</sup> Kamana rehema ya Mwenyezimungu iwesukira, ija kuwavusha wanu piya. <sup>12</sup> Julu ya rehema-yo, tífundiwa tase kutowa kutenda ibada pamoja na wájibu wa kibinadamu, ila tiinshi enzi ya rero-yi kwa shariya, tiritunze wanyewe, na tinshugulikire Mwenyezimungu. <sup>13</sup> Kwa javyo tirindira suku yakujanliiwa yatiri nawo tamaa, pausaka kufafanuriwa utukufu wa Nlungu wetu nkulu na Nvushi wetu, Almasihi Insa. <sup>14</sup> Iye ndi aripereke kwa ájili yetu ofwe, ipate atombore mabaya piya na atiswafi, atiture kuwa wanu wake iye mwananyewe, wakushugulikira nfululu vitendo vyema-vyema.

<sup>15</sup> Basi Titu, evi vinu-vi ufunde. Uwarimbise myoyo na uwasutumumu, na mamulaka piya. Usimwase anta munu kukukejeli.

## 3

*Tayari kutenda meema piya*

<sup>1</sup> Sambu, wambire wanu wawenshimu mafalume pamoja na wenye mamulaka, wasikirize, wawe tayari kutenda meema piya, <sup>2</sup> wasintukane munu asaka kuwa onse, warisapuse nkati ya kukaidiyana, wawe na imani, na warinyenyekeye mbere ya wanu piya.

<sup>3</sup> Kamana mida ofwe novyo atikiwa na deretu, atikisikiriza, tîteseka, tikiwa watwana wa wájibu wakunyata jisijisi na vitendo vibaya vikitajibu kutenda. Útijala ucaputu na wiyana, na tîkinana. <sup>4</sup> Fala pavitisukire wema na pendo rakwaminika ra Mwenyezimungu Nvushi wetu, <sup>5</sup> iye kativusha, siyo kwa sababu ya vitendo vya shariya vyatitendire, ila kwa sababu ya huruma yake. Kativusha patoziwe na patipongoriwe upya julu ya Roho Takatifu. <sup>6</sup> Noyo Roho Takatifu-yo, julu ya Insa Almasihi Nvushi wetu, Mwenyezimungu katususira kwa wingi. <sup>7</sup> Kwa kuwa tikwakikishiwa julu ya rehema ya Mwenyezimungu, tiwe wariti wa tamaa ya mainsha a milele. <sup>8</sup> Ewu ndi usemi wakwaminika! Ntamana, vinajibu kuwa evi vinu-vi uwe ukenekezere, ipate wanu wari kuntumaini Mwenyezimungu washugulike wazidi kutenda wema. Evi ndi vyema, vya faida ka wanu piya.

<sup>9</sup> Fala pawakaidiyana wanu vinu savina deretu, au kuhusu waraka ya mazina a wababu zawo, au kuhusu Taureti, au kwawanyana makundi, murisapuse. Vinu-vyo avina faida wala avina mana. <sup>10</sup> Munu akukusalumurira umani, mwambire mara moja au mara mbiri, na akizidi kutenda javyo, mwase. <sup>11</sup> Ijiwa kuwa munu kamba eyo kataiwa shonge, ázidi kukola dambi. Kweli, karilamula hukumu mwananyewe.

*Salamu za mwinsho*

<sup>12</sup> Sambu, panisaka kukuperekera Aritema au Tikiku, tenda fadili uje upesi Nikopoli tiwonane, koma nilangela kwikala noko mirongo ya baridi. <sup>13</sup> Tenda juhudi uwasaidiye nkati ya safari yawo Zena, mwerezi shariya, pamoja na Apolu, ipate wawe nawo piya cawasakula conse. <sup>14</sup> Na wanu wetu warifunde kushugulikira vitendo vyema, wawavye wenzuwawo pawatowiwa na kinu, ipate mainsha awo awe na faida.

<sup>15</sup> Wanu wari nomi kuno piya wakuperekera salamu. Tafadali, wape salamu zangu wenye kwamini wakutipenda. Rehema iwe nomwe piya.

## Waraka ya Paulu ka Filemoni

### Mwanzo

Eyi waraka-yi ikwereza kuhusu kupembezana kati ya wenye kwamini. Onezimu akiwa ntwana wa mwenye kwamini wakwitiwa Filemoni kaya ya Kolosayi. Viwoneka kuwa Onezimu kamwiwira Filemoni, ndimana akitira. Wakati Paulu waakiwa Roma, Onezimu akiwonana na Paulu akilawirira kuwa mwenye kwamini. Paulu kandika eyi waraka-yi kiyasi ca mwaka wa 60 bandi ya Almasihi na akimpa Onezimu asukure ka Filemoni. Paulu kanlebela ampokerere Onezimu kamba nduye kati ya Almasihi, na kampa tamaa kuwa anripa kwa garama yasaka kutumira yonse Onezimu akijuzi awe pamoja na Filemoni.

<sup>1</sup> Omi Paulu, nfungwa kwa kuwa nintumika Almasihi Insa. Eyi waraka-yi, omi pamoja na nduyangu Timotiyu tukuperekera uwe Filemoni, mpendani wetu na ntumisi mwenzetu, <sup>2</sup> na jamati ijumulananga kwako-ko, pamoja na nlumbwetu Afiya, na nduyetu Arikipu atenda vita pamoja nafwe yakwereza Habari Ngema. <sup>3</sup> Mwenyезimungu Baba wetu, na Mwenye Insa Almasihi, wakujanliyenihemba na salama.

<sup>4</sup> Panilebela duwa, daima nukukumbukira, ninshukuru Mwenyезimungu kwako uwe, <sup>5</sup> kwa kuwa nisikira kuwa uwapenda watakatifu piya, na kwankuntumaini Mwenye Insa. <sup>6</sup> Nilebela duwa kuwa uwe uzidi kuwa pamoja nofwe nkati ya kwamini kwako ipate uje wereriwe sana-sana piya vinu vyema-vyema vyatiwa nawo\* kwa kuwa tilungana na Almasihi. <sup>7</sup> Nduyangu, nipata radi nyingi na moyo wangu urimba kwa sababu ya pendo rako, konta uwarimbisa myoyo watakatifu.

<sup>8</sup> Kwa javyo, ingawa nanawo haki julu ya Almasihi yakukwamuru cikulazimire kutenda, <sup>9</sup> fala kwa sababu ya pendo retu, nihitari nukulebele. Sambi, omi Paulu, nuluvaa na niwa nkifungo novyo kwa sababu ya kuntumika Almasihi Insa, <sup>10</sup> nukutafadali kuhusu mwanangu Onezimu, vyanilawirire kuwa babuye konta yakunlongoza ka Almasihi nkalaboshu-mu. <sup>11</sup> Mida, iye aakifai† kinu kwako uwe, fala sambi afai pakulu kwako uwe mpaka kwangu omi novyo. <sup>12</sup> Onezimu nankunludisa aje kwako. Kusema kweli, iye ndi moyo wangu. <sup>13</sup> Vinajibu nikare naye nokuno kanifungiwe kuno kwa sababu ya Habari Ngema, anisaidiye ukosofu wa uwe. <sup>14</sup> Fala sisaka kutenda anta kinu sairi kwa kusaka kwako uwe. Sisaka kuwa unisaidiye ka kukushurutisa, ila kwa radi yako. <sup>15</sup> Dalili iwa anzima ya Mwenyезimungu yakuwa Onezimu akutire suku aba, ipate umpokerere uwe naye milele, <sup>16</sup> siyo kamba ntwana basi, ila novyo kamba nduyetu wakupendiwa. Iye omi nimpenda pakulu, iye kazidi kupendiwa pakulu futi nowe kwa kuwa ntwana na nduyo kati ya Mwenye.

<sup>17</sup> Basi, ukinitula kamba nduyo mwenye kwamini, mpokerere Onezimu kwa namuna mmoja kamba vyaukisaka kunipokerera omi. <sup>18</sup> Uture pambari, ikiwa kakudulumu au ummwira kinu kimojawapo, deni-yo andika zina rangu omi. <sup>19</sup> Omi Paulu nankwandika na nkono wangu mwaneyewe: “Omi nukuripa.” Wala sukwambira kuwa mainsha ako a kiroho nukuwira! <sup>20</sup> Kweli nduyangu, kwa kuwa tilungana na Mwenye, vikinajibu unifai‡ javi: unirimbiwe moyo§ kwa kuwa tinfulata Almasihi! <sup>21</sup> Nitumaini kuwa usikiriza, ndimana nukwandikira. Nukwijiwa kuwa utenda vyanukulebele, na upundisa!

<sup>22</sup> Nukulebela novyo kuwa unitengezere kisusi kimoja, konta, julu ya duwa zenu, nanawo tamaa kuwa iwapo nafasi nukuwa pamoja namwe.

<sup>23</sup> Epáfora tiwa onse nkalaboshu-mu kwa sababu yakuntumika Almasihi Insa, neye akuperekerani salamu. <sup>24</sup> Na wenzangu nkati ya kazi yetu, Maruku, Arishitariku, Dema, pamoja na Luka, ewo wakuperekerani salamu.

<sup>25</sup> Rehema ya Mwenye Insa Almasihi iwe pamoja namwe.

\* 1:6 Au: “vyatikidiri kutenda”. † 1:11 Zina ra Onezimu mana ake “aafai kinu”. ‡ 1:20 Paulu aseza na semo “kufai” konta “Onezimu” mana ake “kufai”. § 1:20 Ona aya ya 7.

## Waraka ka Waebraniya

Mwanzo

Eyi waraka-yi yandikiwa ipate iwape nguvu wenye kwamini wakati wa tafauti. Ikolota kuwa Insa Almasihi ndi bora pakulu koliko piya wengine, na katenda piya vikisakikana ipate atipereke ka Mwenyezimungu.

Wandikiriwa Mayahudi wakifulatanga Insa ipate warifunde vinu viripo nkati ya dini yawo (vinu kamba-vi: kutenda kafara, walongozi wa dini, na Nyumba Takatifu) na tabiya ya kuinshi mainsha mapya nkati ya kunfulata Insa. Eyi Waraka-yi itolotera kuwa Mwenye Insa Almasihi kweli-kwelini ndi nlongozi wa dini wa mana, na ndi awere kafara kamili ilaviwe mara moja basi, kwa daima milele, ipate itombore kifungo ca dambi zetu. Iye kamilifu na atenda vyaasaka Mwenyezimungu. Aasakurikana tena munu mwengine wakutivusha na átipa mainsha a milele.

*Mwana wa Mwenyezimungu nkulu pakulu*

<sup>1</sup> Mida-na-midada, Mwenyezimungu kâsowera na wababu zetu mara nyingi zawenye, kwa namuna nyingi zawenye, julu ya minabii. <sup>2</sup> Fala sambi, suku za mwinsho-zi, kasowera nofwe julu ya Mwanawe, aturiwe na Mwenyezimungu kuwa mwenyé irati wa vinu piya, na iye ndi ire julu yake Mwenyezimungu ombire vinu piya. <sup>3</sup> Mwana-yo ndi nlangaza wa utukufu wa Mwenyezimungu, na atolotera kweli-kwelini vyaari Mwenyezimungu. Vinu piya mulumwengu-mu viwankwikala kwa uwezo wa ámuri zake. Bandi yakutimiza kazi yake yakuswafi madambi, kekala nkono-nriro wa Mwenye Nkulu mbinguni, <sup>4</sup> kwa kuwa kantula kuwa bora pakulu sana zaida ya malaika, kamba zina raritire rakuwa na mamulaka pakulu zaida ya mazina a malaika.

<sup>5</sup> Ndi kweli konta Mwenyezimungu tangu aanamwambira laika wake mmojawapo javi\*:

“Uwe kuwa mwanangu,  
omi rero nanza kuwa wawayo.”

Na tena, aanamwambira laika mmojawapo javi†:

“Omi nukuja kuwa Baba wako  
na uwe ukuja kuwa mwanangu.”

<sup>6</sup> Visitoshe Mwenyezimungu, paawere tayari kumpereka Mwanawe ntanzi‡ mu-  
lumwengu-mu, kaamba§:

“Piya malaika wa Mwenyezimungu wamwabudu.”

<sup>7</sup> Kuhusu malaika kaamba javi\*:

“Mwenyezimungu awatenda malaika wawe kamba mepo,  
watumisi wake wawe kamba malulimi a moto.”

<sup>8</sup> Fala kuhusu Mwanawe, akwamba javi†:

“Uwe Mwenyezimungu, útawala daima milele.

\* 1:5 Ona 2 Samuweli 7:14; Zaburi 2:7. † 1:5 Ona 2 Samuweli 7:14. ‡ 1:6 Ntanzi akiwa nriti wa vinu piya vya wawaye. § 1:6 Ona Kumbukumbu 32:43. \* 1:7 Ona Zaburi 104:4. † 1:8 Ona Zaburi 45:6,7.

Úwatawala wanu muufalume wako kwa shariya.  
<sup>9</sup> Kwankupenda ukamilifu na wankukukima ubaya.  
 Kwa javyo, omi Mwenyezimungu, Nlungu wako,  
 nukumiminirani mafuta a radi  
 pakulu koliko wenziwo piya.”

<sup>10</sup> Mwenyezimungu kamwambira Mwanawe tena‡:

“Mwenye, tangu mwanzo,  
 uwe ndi uturire aluserusu ya duniya,  
 na kwa makono ako kumba bingu piya.  
<sup>11</sup> Evyo piya-vyo vilainika, fala uwe kuwapo daima.  
 Avija kufai kinu, kamba nguwo zakupapuka.  
<sup>12</sup> Kamba zubau ya mida, ndi vyauja kukunja,  
 kamba munu vyaaluriza nguwo, uwapindula.  
 Fala uwe ndi nowe wa daima,  
 kuinshi kwako akuna mwinsho.”

<sup>13</sup> Mwenyezimungu laikani wamwambire suku moja javi§:

“Ikala mahala bora-pa upande wangu wa nkono nriro-wu,  
 mpaka maaduwi wako niwature kumaulu kwako”?

Malaika-wo wa kinani? <sup>14</sup> Piya-wo siroho zintumika Mwenyezimungu na awaperekiwe kuwasaidiya wanu waja kuvushiwa?

## 2

### *Nafasi ulu yakuvushiwa*

<sup>1</sup> Ndimana, tijuzi titengemane tifulate pakulu vyatisikira ipate tisipoteye. <sup>2</sup> Kamana habari zereziwe na malaika zoloka, watupa shariya onse na wabishi wapata hukumu iwajuzire <sup>3</sup> Kwa javyo, futi ofwe ikiwa atiyeriwa tisaka kunusurikaja na kuvushiwa kukulu-ko? Kuvushiwa-ko ndi kwanzire kwereziwa na Mwenye mwaneyewe, ikisa wasikire watakikisha kuwa kweli. <sup>4</sup> Mwenyezimungu neye novyo azidi kwakikisha kuwa habari-zo zakweli julu ya alama, matajabisa, maajuza a uwezo jisijisi, na julu yakutisusira uwezo wa Roho Takatifu, sawa-sawa na vyaasaka mwaneyewe.

### *Insa Almasihi afungula njira tivushiwe*

<sup>5</sup> Mwenyezimungu aawapere malaika uwezo wakitawala ulumwengu mupya\* watamba-wu. <sup>6</sup> Fala mMandiko Matakatifu mamojawapo† kalavya ushahidi javi:

“Yarabi Mwenyezimungu,  
 binadamu nani wakummwaza?  
 Binadamu akuyeri kakinani?  
<sup>7</sup> Kuntula utoto aba kawa sini ya malaika,  
 kunkonga lemba ra utukufu na inshima,  
<sup>8</sup> kutula piya sini ya kumaulu kwake.”

Sambi, payambiwa kuwa “kutula piya sini yake”,  
 mana ake ndi kuwa acipo anta kimoja saciri sini yake.  
 Fala sambi-pa wanu atiri kuwawona piya sini yake.

<sup>9</sup> Ila tankummona iye kuwa, kwa wakati aba, katuriwa utoto koliko malaika. Iye Insa ndi ayerere kifo, julu ya rehema ya Mwenyezimungu, kwa ajili ya wanu piya. Ingawa

‡ 1:10 Ona Zaburi 102:25-27. § 1:13 Ona Zaburi 110:1. \* 2:5 Ulumwengu mupya ndi namuna nyengine zawaja kuinshi wenye kuvushiwa na Insa. † 2:6 Zaburi 8:4-6.

kâturiwa utoto, fala sambi-pa, kwa sababu ya kutabika ka kifo, iye kakongiwa lemba ra utukufu na swifa!

<sup>10</sup> Kamana iwapo shariya kuwa Mwenyezimungu, mwenyé vinu piya na mwenyé kumba piya, aje nawo wafulati wengi wawe upande wa utukufu wake. Katenda javyo julu ya kunteza Insa, awalóngoza wanu kuwavusha, awe kamilifu julu ya kutabika.

<sup>11</sup> Kamana ire atakátifu, na ware watakatífiwa, walawirira ka Baba mmoja. Ndimana Insa aawona haya kuweta “wanduzangu”, <sup>12</sup> kamba vyayambiwe mMandiko‡:

“Níwerezá baina vyautendanga uwe wanduzangu.  
Nukwimba nukukusifu mbere ya wanu wako.”

<sup>13</sup> Mmandiko mengine, iye kaamba javi§:

“Omi níntumaini Mwenyezimungu.”

Ikisa kaamba tena:

“Niwa epa, na ware Mwenyezimungu waunaminire kuwasunga,  
ewo wawa kamba wanangu.”

<sup>14</sup> Sambu, ware wetiwe wanawe na Insa, kwa kuwa ewo binadamu\*, iye mwananyewe kâlawirira kwa namuna moja ipate julu ya kifo cake, anshinde ire ári na uwezo wa kifo, Ibilisi. <sup>15</sup> Kwa namuna-yo, piya wákiwa watwana kwa milele kwa sababu ya kopa kufwa, Insa kawanusuru. <sup>16</sup> Kamana vikwijiwikana kuwa aajire kuwasaidiya malaika, ila kâja kusaidiya ujukulu wa Iburahima. <sup>17</sup> Ndimana neye akijuzi awe sawa-sawa na wanduze kwa kila namuna, ipate awe nlongozi nkulu wa dini wakuwa ndi mwenyé huruma na mwaminifu. Kwa namuna-yo, antumike Mwenyezimungu, iye mwananyewe awe kafara, ipate madambi a wanu aswamiiwe. <sup>18</sup> Kamana, kwa kuwa katabika julu ya kushetwaniwa, iye kanawo uwezo wa kuwasaidiya ware wenye kushetwaniwa.

### 3

#### *Insa ndi nkulu zaida ya Musa*

<sup>1</sup> Kwa javyo umwe, wanduzangu watakatifu, wenzangu titiwe mbinguni, akuyerini Insa. Iye ndi walii na nlongozi wetu nkulu wa dini yatiri kwereza-yi. <sup>2</sup> Kamba Musa vyaákiwa mwaminifu na kazi yake nnyumba ya Mwenyezimungu\*, na Insa ákiwa mwaminifu ka Mwenyezimungu mwenyé kuntondola. <sup>3</sup> Musa kasifiwa, fala Insa kawoniwa kuwa ndi wakujúzi kusifiwa pakulu zaida ya iye, kamba njengi wa nyumba vyaasifiwa pakulu koliko nyumba yawenye. <sup>4</sup> Kamana kila nyumba ítengeziwa na munu, ila atengéza vinu piya Mwenyezimungu. <sup>5</sup> Musa ákiwa ntumisi mwaminifu nnyumba ya Mwenyezimungu piya, kalavya ushahidi wa vire vikija kwereziwa mbere. <sup>6</sup> Fala Insa Almasihi mwaminifu kamba mwana, amiri wa nyumba-yo. Na nyumba-yo ndufwe, ikíwa tizídi koloka mpaka mwinsho, na hakika na kwamini nkati ya tamaa yatirindira.

#### *Ukosofu wa kutowa kwamini*

<sup>7</sup> Kwa javyo, kamba vyaamba Roho Takatifu† javi:

“Rero, mukisikira shauti ya Mwenyezimungu,

<sup>8</sup> myoyo yenu musitaye ugumu,  
kamba wababu zenu pawábishane nami,  
suku yawâniyerere nlanga.

<sup>9</sup> Emo wababu zenu wâniyerera waniwone canikisaka kutenda,

‡ 2:12 Ona Zaburi 22:22. § 2:13 Ona Izaya 8:17. \* 2:14 Kigeregu: “wanawo nyama na damu”. \* 3:2 “Nnyumba ya Mwenyezimungu” mana ake “nkati ya Mwenyezimungu”. † 3:7 Ona Zaburi 95:7-11.

ingawa wâwona vyaniwasaidiye muda wa myaka arubaini.

<sup>10</sup> Ndimana níkimiwa na noco kizazi-co, nikisowera javi:

‘Daima wankukosa mmyoyo mwawo,  
wakatala kufulata njira zangu.’

<sup>11</sup> Kamba vyanílapire paníkimiwe, nikamba:

‘Awaja kwingira mahala pangu papumuzi.’ ”

<sup>12</sup> Wanduzangu, more-more asilawirire munu nkati yenu wakuwa na moyo mbaya wakutowa kwamini, wakulongoza kukatala kunfulata Nlungu hai. <sup>13</sup> Kwasa javyo, zidini kurimbisana myoyo kila suku sambi nopa pamwitiwe-pa, ipate asilawirire nkati yenu munu wakutaiwa moyo ngumu, wakuteseka na dambi. <sup>14</sup> Kamana kwamini kwetu katiwere nawo tangu mwanzo, tikizidi koloka mpaka mwinsho, tilawirira kuwa wenziwe Almasihi nkati ya kazi yake. <sup>15</sup> Ndi kamba vyayambiwe<sup>‡</sup>:

“Rero, mukisikira shauti ya Mwenyezimungu,  
myoyo yenu musitaye ugumu,  
kamba wababu zenu pawâbishane nami.”

<sup>16</sup> Epa wasikire shauti ya Mwenyezimungu wakibishana naye ndi wepi? Kusema kweli, sipiya walongoziwe na Musa kulawa Miswiri? <sup>17</sup> Na ware Mwenyezimungu waakimiyane nawo muda wa myaka arubaini ndi wepi? Siware wakorire dambi, wakifwira nlanga nomo? <sup>18</sup> Na paalapire kuwa “awaja kwingira mahala pangu papumuzi”, waakiwamba ndi wepi? Siware watupire kauli zake? <sup>19</sup> Basi, tereriwa kuwa awakidirire kwingira kwa sababu ya kutowa kutumaini.

#### 4

<sup>1</sup> Kwa kuwa tanawo mpaka sambi-pa tamaa yakwingira mahala pake papumuzi, tiritunze sana-sana ipate asilawirire mmoja wenu wakusokerera kwingira nopo mahala-po. <sup>2</sup> Kamana teréziwa Habari Ngema kamba vyawereziwe ewo\*, ila ewo cawasikire aciwafaire kinu, kwa kuwatowa umoja wa kwamini cawasikire. <sup>3</sup> Basi, ofwe wenye kwamini tingira nopo mahala papumuzi-po, kamba vyaâmbire Mwenyezimungu javi<sup>†</sup>:

“Kamba vyanilapire nkati ya nyongo yangu:  
‘Awaja kwingira mahala pangu papumuzi.’ ”

Kasowera javyo ingawa kazi yake kâtimiza tangu pawisire kumbiwa ulumwengu.

<sup>4</sup> Kamana kuhusu suku yasaba, nsitari mmoja wa Mandiko<sup>‡</sup> ukwamba javi:

“Suku yasaba Mwenyezimungu kapumula kwa kutimiza kazi zake piya.”

<sup>5</sup> Usowezi mmoja nowo uwiriziwa tena:

“Awashubutu kwingira mahala pangu papumuzi.”

<sup>6</sup> Kwa kuwa wanzire kwereziwa Habari Ngema awengire kwa kutowa kusikiriza, wengine wapewa nafasi yakwingira nopo mahala papumuzi-po. <sup>7</sup> Tukwijiwa kinu kamba-ci konta Mwenyezimungu katula suku nyengine, kaamba kuwa ndi suku ya “rero” pairipo nafasi yakwingira mahala papumuzi-po. Kwa myaka mingi ipitire, Mwenyezimungu kâsowera julu ya Daudi, kamba vyaamba futi:

“Rero mukisikira shauti ya Mwenyezimungu,  
myoyo yenu musitaye ugumu.”

<sup>‡</sup> 3:15 Ona Zaburi 95:7; Waebraniya 3:7. \* 4:2 “Ewo” ndi ware wâkiwa nlanga. <sup>†</sup> 4:3 Ona Zaburi 95:11. <sup>‡</sup> 4:4 Ona Mwanzo 2:2.



<sup>8</sup> Kamana inawa Yoshwa wanu-wo kawalongoza mahala papumuzi, aikibidi Mwenyezimungu kusowera tena, kutula suku nyengine. <sup>9</sup> Kwa javyo, kamba Mwenyezimungu vyaapumure suku yasaba pesire kumba ulumwengu, ingaripo nafasi ya wanu wa Mwenyezimungu kupumula. <sup>10</sup> Kamana mwenyé kwingira mahala papumuzi pa Mwenyezimungu apumula kazi zake sawa-sawa vyaapumure Mwenyezimungu kazi zake.

<sup>11</sup> Basi, mahala papumuzi-po, titende juhudi tingire, ipate asiwepo wakunkuna kamba vyaviwakunire mida, wakutowa kwingira kwa sababu ya ubishi.

<sup>12</sup> Kamana usemi wa Mwenyezimungu uwa nawo uhai na nguvu, unoréka pakulu kupunda jambiya yakusinja kuno na kuno. Úpitirira mpaka mmoyo, ukwawanya moyo na roho kamba jambiya vyayawanya nyama na makongolo. Ndimana usemi wa Mwenyezimungu úkidiri kwawanya mawazo meema na mabaya a mmoyo. <sup>13</sup> Aapo kiyumbe akidiri kufisa siiri mbere ya Mwenyezimungu. Kwake iye, piya viwa paweru, awona vinu piya na maso ake. Na vitendo vyatitenda tijuzi kunjibu.

#### *Insa atipendeleya mbere ya Mwenyezimungu*

<sup>14</sup> Sambu, kwa kuwa tanawo nkulungwa nkulu wa dini atangurire binguni, Insa, Mwana wa Mwenyezimungu<sup>§</sup>, tukeni tikore makono mawiri kwamini kwetu katereze.

<sup>15</sup> Kamana nlongozi wetu nkulu wa dini akidiri kutiwonera utungu ufuko wetu, kwa kuwa kashetwaniwa kwa namuna-zi piya kamba vyatishetwaniwa ofwe, ila iye aakorire dambi.

<sup>16</sup> Basi, tukeni na uhakika tiwe karibu na kiti ca Mwenyezimungu, tipate huruma na rehema patisakula kusaidiwa.

## 5

<sup>1</sup> Kila nkulu wa wakulungwa wa dini ákitondoriwa nkati ya wanu, akitawaziwa ipate antumike Mwenyezimungu kwa faida ya wanu. Kazi yake íkiwa yakupereka kafara na swadaka ipate wanu wafutiwe madambi awo. <sup>2</sup> Watikínifu na sawári makamilifu, iye ákidiri kuwawonera utungu, kwa kuwa iye mwananyewe kaveya. <sup>3</sup> Kwa javyo, ájuzi apereke kafara kwa madambi ake iye mwananyewe kamba vyaalavya kafara kwa madambi a wanu wengine. <sup>4</sup> Na hapana munu wakuritawaza mwananyewe cewo cakusifiwa-ci, ila akolotiwa na Mwenyezimungu kamba vyavínkunire Aruna.

<sup>5</sup> Kwa namuna moja noyo, Almasihi aaritawaze iye mwananyewe ubora wakuwa nkulungwa wa dini. Ila Mwenyezimungu kantondola, akimwambira\*:

“Uwe kuwa mwanangu,  
rero omi nukupongola.”

<sup>6</sup> Na mahala pengine<sup>†</sup>, akwamba tena javi:

“Ukuwa nlongozi wa dini wa milele,  
kamba vyaawere Melkizideki.”

<sup>7</sup> Insa, mainsha ake mulumwengu-mu, akilebelanga duwa ka Mwenyezimungu, mwenyé uwezo wakunvusha nkati ya kifo. Akilebelanga kwa shauti ulu-ulu kuno akinlawo masozi. Na akisikiriziwa kwa sababu ya kunyenyekeya kwake kutenda vyaasaka Mwenyezimungu. <sup>8</sup> Ingawa ákiwa mwana, karifunda kutwii julu ya tabu zimpatire. <sup>9</sup> Na paatimize vinlazimire kutenda, kalawirira kuwa Nvushi wa milele wa piya wenye kunfulata. <sup>10</sup> Na Mwenyezimungu kantula kuwa nkulu wa wakulungwa wa dini, kwa namuna moja noyo kamba vyaákiwa Melkizideki.

#### *Usase kuntumaini Insa Almasihi*

<sup>§</sup> 4:14 “Mwana wa Mwenyezimungu” ndi zina rimojawapo retiwa Insa. Rikolota kupatana kwema ka Insa na Mwenyezimungu, kamba mwana na wawaye. Eri zina-ri aisema kuwa cipita kitendo ca muka na nlume, ila kupatana kukulu ka kiroho. \* 5:5 Ona Zaburi 2:7. † 5:6 Ona Zaburi 110:4.

<sup>11</sup> Kuhusu ewu mwaha-wu<sup>‡</sup>, tanawo vinu vingi vyawenye vyakukwerezani. Fala virigariga kukwerezani konta amusaka kwereriwa. <sup>12</sup> Kamana, ingawa upita wakati mwingi, mujuzi muwe wanlimu, fala munsakula munu akufundeni vinu vyakwanza vya habari za Mwenyezimungu. Muwa kamba watoto musakula kujiji maziwa, iri hali mukijuzi murye cakurya cakukamatiwa. <sup>13</sup> Kamana ajúzi kunywa maziwa onse angari toto, ndi sejiwa cema. <sup>14</sup> Fala cakurya cakukamatiwa ndi cankulungwa. Kwa njira ya kufundiwa, ewo wanawo ankili yakutondola cema na kibaya.

## 6

<sup>1</sup> Kwa javyo, tase vyatanzire kurifunda kuhusu Almasihi, tukeni mbere mpaka tifikirire vyakurifunda vyakukamilika. Tisijenge tena upya aliserusu zakufulata ngano kamba ezi: cakwanza, ibidi kutubiya vitendo vyakuja na kifo, na kurimbirira kuntumaini Mwenyezimungu;

<sup>2</sup> capiri, kufunda kuhusu koza, alama ya kutubiya;

catatu, kuntula munu makono;  
caane, kuwafufula wanu ka wafwi;  
na catanu, kulamuriwa ka milele.

<sup>3</sup> Nevyo, Mwenyezimungu akisaka, titenda.

<sup>4</sup> Kamana ware wasire kunkubali Insa, aapo akidiri kuwaludisira kutubiya tena upya. Ewo mara moja wâpokerera nuru ya Mwenyezimungu, wâyeza thawabu ya binguni, wâpokerera Roho Takatifu pamoja na wenziwawo. <sup>5</sup> Wâyerera wema wa usemi wa Mwenyezimungu, na wâyerera vitendo vya uwezo visaka kukuna paaja kutawala Mwenyezimungu. <sup>6</sup> Fala novyo-sivyo, wantula minyongo iye! Aapo akidiri kuwaludisira kutubiya tena, konta wankejeli baina Mwana wa Mwenyezimungu, wangomezera tena mpaka warihukumu.

<sup>7</sup> Kamana ewo wawa kamba ardhi inywa maji a nvula painya ponse. Ikiwa ardhi-yo iruwerya miti ya kuwafâi warimi, ardhi-yo ijanliiwa na Mwenyezimungu. <sup>8</sup> Fala ikiwa ardhi-yo iruwerya miti ya miwa na mbiriwiri, saifâi na karibu yakulaniwa. Ardhi-yo mwinshoni ikociwa.

\* 3:6 Lulimi rilandanisiwa na moto konta ridangula, aapo munu akidiri kumiliki lulimi rake. † 3:6 Ibilisi. ‡ 3:9 Ona Mwanzo 1:27. Mwenyezimungu kawomba wanu wanlande iye mwaneyewe, ndimana namuna vyatiwatafiti wanu wengine ndi namuna vyatintafiti Mwenyezimungu mwaneyewe. § 3:12 Mana ake ndi kuwa usowezi mwema aulawa mmoyo wakunyata.

<sup>1</sup> Kubishana na umani kati yenu umwe vilawirira ndepi? Cisalamula siwájibu mbaya úri kumana mmyoyo mwenu? <sup>2</sup> Cukwajibuni kinu samuna, ndimana mukulaya\*. Muwa nawo wivu, fala amupata camusakula, ndimana mutenda umani na vita. Kweli-kwelini, amuna kwa kuwa amulebela. <sup>3</sup> Na mukilebela, amupewa, konta mulebela na niya mbaya. Musakula kupata vinu ipate mutimize wájibu wenu mbaya tu basi.

<sup>4</sup> Umwe wazinzi! Amwijiwa kuwa mukiwa marafiki wa vinu vya mulumwengu-mu, mukuwa maaduwi wa Mwenyezimungu? Basi, ikiwa niya yenu ndi ya urafiki wa vinu vya mulumwengu, mukuwa maaduwi wa Mwenyezimungu. <sup>5</sup> Au muwaza kuwa Mandiko asema bure paamba javi:

“Roho Takatifu ari mmyoyo mwetu atiririra wivu.†”

<sup>6</sup> Novyo-sivyo, iye atipa rehema pakulu. Kamba vyaamba Mandiko:

“Wenye kuridāi Mwenyezimungu ashindana nawo, fala wenye kurinyenyekeya awapa rehema.”

<sup>7</sup> Kwa javyo, tendani vyaasaka Mwenyezimungu. Nshindeni Ibilisi, na iye akutirani. <sup>8</sup> Ritengezeni muwe karibu ya Mwenyezimungu, na iye akuwa karibu namwe umwe wamadambi, asani kutenda ubaya‡. Umwe wanu wa malulimi mawiri, swafini myoyo yenu§. <sup>9</sup> Uzunikani, tubiyani na rirani. Kiseko cenu-co citaduke kiriro, radi yenu itaduke uzuni. <sup>10</sup> Basi, rinyenyekeyeni mbere ya Mwenye, na iye akuja kukutulani mahala paswifa.

#### *Musiwalaumu wenzenu*

<sup>11</sup> Wanduzangu, musiwalaumu wenzenu. Munu ansowérera caputu au anlaúmu nduye, asowerera caputu Taureti, kankulaumu noyo Taureti-yo. Ukilaumu Taureti, auri nfulati wa Taureti ila kuwa mwenyé kulamura. <sup>12</sup> Kawapo mmoja tu basi esuse Taureti, na ári na haki ya kulaumu. Iye ndi ári na uwezo wakuvusha na wakudangula. Basi, uwe kuwa nani wakunlaumu mwenziwo?

#### *Usiritumaini mwaneyewe*

<sup>13</sup> Sikirizani, umwe mwâmba javi: “Rero au makeso, tikuka mahala kada, tikekare mwaka mmoja noko, tikicuruza tipate nzuruku mwingi.” <sup>14</sup> Cisaka kukukunani umwe makeso, mukwijiwa? Mainsha enu akuwa mwaja? Kamana muwa kamba nambwe, ikuwepo wakati aba, ikisa aiwepo. <sup>15</sup> Kwasa javyo, nanga mwangibiza javi: “Mwenyezimungu akitijanliya, tukuwa hai, titenda kinu-kada au kinu-kada.” <sup>16</sup> Fala umwe muridāi na murisukula. Evyo vitendo-vyo piya vibaya. <sup>17</sup> Basi, munu wakwijiwa cema caajuzi kutenda fala akitowa kutenda, ndi dambi kwake iye.

## 5

#### *Vyakuwalaizira matajiri wakuwatabisha wanu wengine*

<sup>1</sup> Sikirizani umwe matajiri, rirani na rishukuni kwa sababu ya tabu zakofya zija kukupatani. <sup>2</sup> Mali enu avunda, na nguwo zenu zitafuniwa na mabarada. <sup>3</sup> Oru na parata yenu viwota ange. Ange-yo ikuja kuwa ushahidi wakukukaidini, ikuja kukapira mwiri wenu kamba moto vyawoca. Suku za mwinsho-zi, muriturira mali mengi awenye. <sup>4</sup> Fala sikirani! Sikirani kiriro ca wakazi wenu wakivunanga vyakurya vyenu, konta nshahara wawo auwere wa shariya! Kiriro ca wavuni cinfika Mwenyé Uwezo. <sup>5</sup> Umwe nkati ya mainsha enu mulumwengu-mu muvuza, mutimiza piya vyakukwajibuni. Múkiwa kamba makondoo vyawarya vyawasaka, wakinenepa, sawejiwa kuwa ndi suku ya kusinjiwa. <sup>6</sup> Muwahukumu na muwolaya wenye shariya sawabishane namwe.

#### *Kuvumirira nkati ya tabu*

\* 4:2 Ona Matwaya 5:21,22. † 4:5 Namuna nyengine yakwereriwa haya-yi ndi javi: (i) Mwenyezimungu aririra wivu roho zetu mmyoyo mwetu. (ii) Roho zetu na mmyoyo mwetu uwapo wájibu mbaya. ‡ 4:8 Kigeregu: “nawani mmakono”. § 4:8 “Swafini myoyo yenu” mana ake mwase mawazo mabaya.



<sup>7</sup> Wanduzangu, vumirirani pamurindira kuja ka Mwenye. Nkumbukireni nrimi vyaarindira visumo vya faida pakulu mmasamba, avumirira mpaka kunya nvula ya kinja na nvula ya kusi. <sup>8</sup> Umwe novyo vumirirani, olosani myoyo yenu, konta kuja ka Mwenye kuwa karibu. <sup>9</sup> Wanduzangu, musidugudane ipate musihukumiwe. Kusema kweli, Mwenye kulamula shariya kafika futi panryango. <sup>10</sup> Fulatani nfano wa minabii\* wakisoweranga kwa zina ra Mwenye. Ewo wavumirira nkati ya tabu zawo. <sup>11</sup> Onani, tiwawalanga kuwa wari heri ndi wenye kuhitamili. Umwe musikira kuvumirira ka Ayuba na mwereriwa anzima ya Mwenye upande wake iye, kuwa iye ndi mwenye huruma na utungu.

<sup>12</sup> Visitoshe, wanduzangu, musilapire bingu wala ardhi wala kinu cisaka kuwa conse. Ikiwa kweli, mwambe “aye”, na ikiwa siyo kweli, mwambe “siyo kweli”. Musilapire ipate musihukumiwe.

*Uwezo wa kulebela duwa ka kwamini*

<sup>13</sup> Kati yenu, kawapo munu ári kutabika? Akiwapo, alebele duwa. Kawapo munu ári radi? Akiwapo, embe nyimbo za zaburi. <sup>14</sup> Kati yenu, kawapo nlwere? Akiwapo, awete wakulungwa wa jamati, wanlebelele duwa kuno wakimpaka mafuta, kwa zina ra Mwenye. <sup>15</sup> Kulebela duwa ka kwamini kumponesa nlwere-yo, Mwenye anlamusa. Na nlwere-yo, akikola dambi mmojawapo, aswamiiwa. <sup>16</sup> Ndimana, erezanani dambi zenu na lebelelanani duwa ipate muponesiwe. Duwa ya mwenye shariya iwa nawo nguvu pakulu, kweli-kwelini ifái. <sup>17</sup> Kwa nfano, Aliyasi ákiwa mwanadamu kamba nofwe, fala paalebele duwa isinye nvula, ainyere tena mulumwengu-mu kwa muda wa myaka mitatu na myezi sita. <sup>18</sup> Ikisa, kalebela duwa tena, nvula yanza kunya, na ardhi iruwerya visumo vyake.

*Kuwasaidiya wanduzetu kuludira njira ya ukweli*

<sup>19</sup> Wanduzangu, ikiwa mmoja wenu kasa njira ya ukweli, akiwapo munu wakunludisira tena upya, <sup>20</sup> kumbukirani javi: munu ansaidiya mmadambi kumwasisa njira yake yakukosa, akuja kuvusha mainsha a mmadambi-yo nkifo, na noyo aswamiiwa madambi mengi.

---

\* 5:10 Kwa nfano, Yusufu, Yereimiya, Daudi.

## Waraka 1 ya Peduru

### Mwanzo

Peduru kawandikira eyi waraka-yi wenye kwamini wakafilike kwa sababu ya kulum-batiwa kwa kwamini kwawo. Iye kawataya nguvu ipate woloke, kwa kuwakumbusira nfano wa Almasihi, mali atiri nawo nkati yake, na tamaa yawari nawo wenye kwamini kuwa aludi ipate awatware awapereke mbinguni.

Habari ya Peduru ndi javi: kuntumaini Mwenye Insa, muwe wenye kunsikiriza anta paiwa kwa kurigariga pakulu, na kuntejemera kwenu kuwe ka tamaa ya Mwenyezimungu ka kuwa mwinsho átombola. Kutabika kulungana upande wa mainsha etu mulumwengu, fala iye awajanliya mbere ware wantumaini iye.

Peduru kandika eyi waraka-yi kiyasi ca mwaka 65 bandi ya Almasihi.

### *Salamu*

<sup>1</sup> Omi Peduru. Niwa walii wa Insa Almasihi, niwandikira eyi waraka-yi wanu waton-doriwe na Mwenyezimungu, watawanyike porovinsiya za Pontu, Galata, Kapadokiya, Aziya pamoja na Bitaniya. <sup>2</sup> Tangu mida anzima ya Mwenyezimungu Baba wetu íkiwa ya kukutondolani, na Roho Takatifu kâkutulani kuwa watakatifu, ipate muswafiwe na damu ya Insa Almasihi na munsikirize.

Umwe mongeziwe rehema na salama!

### *Kuinshi kwa kutumaini tamaa ya Mwenyezimungu*

<sup>3</sup> Asifiwe Mwenyezimungu, Baba wa Mwenye wetu Insa Almasihi! Kwa huruma zake nyingi, iye katipa nroho zetu mainsha mapya ipate julu ya kufufuka ka Insa Almasihi ka wafwi, tiwe nawo tamaa ya kuinshi milele, <sup>4</sup> na kuriti irati saifujika, saina noda na saipoteya faida yake, ituriwe binguni iwe yenu. <sup>5</sup> Umwe, kwa kuwa mumwamini Mwenyezimungu, mukengeriwa na uwezo wake mupate kuvushiwa, kuri tayari kolotiwa suku za mwinsho. <sup>6</sup> Kwa javyo, ingawa dalili isakikana muuzunike suku aba kwa kutabika jisijisi, fala tendani radi! <sup>7</sup> Eko kutabika-ko kukwakikisha faida ya kwamini kwenu, vyakuri na faida pakulu koliko oru. Oru, ingawa ilainika, iswafiwa na moto. Kwa namuna mmoja noyo, kwamini kwenu kukwakikishiwa ipate kukujisireni swifa, utukufu, na inshima suku yaasaka koolotiwa Insa Almasihi mulumwengu-mu. <sup>8</sup> Ingawa iye amummonire, fala mumpenda. Na ámuri kummona, fala mwankumwamini, na mupata radi yakwijaziwa na utukufu, anta munu ejiwa namuna yakwerezwa, <sup>9</sup> mufurahi konta múpata anzima ya kwamini kwenu, roho zenu zivushiwa.

<sup>10</sup> Kuhusu kuvushiwa-ko, minabii weréze rehema yamuja kupokerera umwe, wasakula na wadairi wereriwe namuna yake. <sup>11</sup> Wakisaka wawonerere mana a cire cawakambiriwa na Roho ya Almasihi nkati yawo, pawakibushuru kuhusu kutabika kaakijuzi kuvumirira Almasihi, na utukufu ukija kunfulata. Wakisakula wejiwe wakatini na nani wavisaka kunkuna. <sup>12</sup> Wafafanuririwa kuwa mambo-yo aakuna ewo wari hai, ila wakati watiri ofwe-wu! Na sambipa noyo habari-yo mwereziwa umwe, julu ya ware wakukwerezani Habari Ngema, kwa uwezo wa Roho Takatifu aperekiwe kulawa binguni. Vija kukunavyo, anta malaika newo viwajibu kutunza wejiwe.

### *Kuinshi na utakatifu*

<sup>13</sup> Ndimana, tengezani ankili yenu muwe tayari. Risungeni wanyewe, na muzidi kutumaini nfululu tamaa ya rehema zamusaka kupewa, suku yaasaka koolotiwa Insa Almasihi mulumwengu-mu. <sup>14</sup> Muwe kamba wasimana wasikiriza, musifulate wájiibu wenu mbaya wa mida wa ujinga wenu. <sup>15</sup> Fala kamba Mwenyezimungu akutondoreni vyaari takatifu, nomwe novyo muwe watakatifu kwa piya vinu vyamutenda. <sup>16</sup> Konta vyandikiwa javi:

“Muwe takatifu konta omi niwa takatifu.”

<sup>17</sup> Pamulebela duwa, mwankumwita “Baba” ire alamúla sannang'aniza munu caari, ila alamula kwa vitendo vya kila munu. Kwa javyo, pamwikala mulumwengu-mu kamba wayeni, inshini kwa namuna yakumwinshimu. <sup>18</sup> Mukwijiwa kuwa momboriwa nkati ya mainsha safái amuritire ka wababu zenu, aiwere julu ya kuripa vinu vyakulainika kamba parata au oru, <sup>19</sup> ila julu ya beyi ya faida pakulu, damu ya Almasihi. Iye ákiwa kamba kondoo saana baka wala saabadilike. <sup>20</sup> Iye katondoriwa atimize eyi anzima-yi tangu ulumwengu saunombiwa, fala tarehe za mwinsho-zi kolotiwa kwa faida yenu. <sup>21</sup> Julu yake, umwe mumwamini Mwenyezimungu, anfufure iye nkifo na antukuze, ipate kwamini kwenu na tamaa yenu iwe ka Mwenyezimungu.

<sup>22</sup> Sambu, kwa kuwa umwe\* muswafiwa julu ya kifulata ukweli, mwankupendana kweli-kweli. Kwa javyo, zidini kupendana kwa niya na ka myoyo swafi. <sup>23</sup> Mupendane javyo kwa kuwa mupongoriwa tena upya, siyo julu ya mbeyu yakulainika ila kwa mbeyu sailainika, julu ya usemi wa Mwenyezimungu uínshi na uri na ukweli daima. <sup>24</sup> Kamba vyavyandikiwe javi:

“Wanu piya wawa kamba minyani,  
ubóra wa munu upunguka upesi kamba wema wa luwa rakuvalaluka.

Nyani ukumiliya na luwa rikugwa,  
<sup>25</sup> fala usemi wa Mola ukwikala milele.”

Na nowo usemi-wo ndi Habari Ngema yamwereziwe umwe.

## 2

<sup>1</sup> Ndimana, julu ya kwasa piya ubaya na piya ulongo, unafiki, wivu, na kufezeyi ka kila namuna piya, <sup>2</sup> akwajibuni maziwa\* kamili, kamba watoto wakupongoriwa sambu. Kwa javyo múkula sana-sana, na múpata kuvushiwa. <sup>3</sup> Mwakikisha futi kuwa Mwenye Insa ndi wema, sinovyo?

### *Almasihi ndi riwe maalumu*

<sup>4</sup> Almasihi ndi riwe hai, kákatariwa na wanu, fala kanawo faida pakulu mbere ya Mwenyezimungu antondore iye. Pamunfika karibu yake, <sup>5</sup> umwe wanyewe muwe kamba mawe hai akujengeriwa nyumba takatifu ya Roho Takatifu ipate muwe walongozi watakatifu wa dini, mupereke kafara za kiroho zakumwajibu Mwenyezimungu, kwa cire caatendire Insa Almasihi. <sup>6</sup> Kamana Mandiko akwamba javi:

“Ona, omi nitula riwe rimoja Yerusalemu†,  
bora sana rítondoriwe kuwa maalumu ra pamembe ya nyumba.  
Na mwenyé kwamini noro riwe-ro aashubutu kuwona haya.”

<sup>7</sup> Kwenu umwe wenye kwamini, ero riwe-ro‡ ra faida pakulu. Fala ka ware sawamini,  
“Riwe rawakatara wajengi

ero rilawirira kuwa riwe maalumu ra pamembe ya nyumba.”

<sup>8</sup> Na:

“Ero ndi riwe rakuwakwakurisa wanu wamojawapo,  
riwe risáka kuwagwisa wanu.”

Ewo wákwakula konta awasikiriza usemi wa Mwenyezimungu, ewo watuririwa viwakune javyo.

<sup>9</sup> Fala umwe ndi kabila itondoriwe, ufalume wa walongozi wa dini, taifa takatifu, wanu watondoriwe wawe wa Mwenyezimungu mwananyewe, ipate mwereze wema nkulu wa ire akwitireni mulawe nkisi, mwingire nnuru yake ya matajabisa.

<sup>10</sup> “Mida umwe amuwere umati wa Mwenyezimungu,

fala epa sambu muwa umati wa Mwenyezimungu.

Mida amuwonire huruma ya Mwenyezimungu,

fala epa sambu muwona huruma yake.”

\* 1:22 Kigeregu: “roho zenu”. \* 2:2 “Maziwa” epa mana ake inlimu. † 2:6 Kigeregu: “Ziyoni”. ‡ 2:7 Riwe-ro rikolota Insa.

<sup>11</sup> Wapendani wangu, kwa kuwa muwa wayeni wakupita mulumwengu-mu, tanukani wájibu mbaya wa kibinadamu, uténda vita na myoyo yenu-yo. <sup>12</sup> Inshini kwa namuna ngema mbere ya wanu sawamwijiwa Mwenyezimungu, ingawa wakulongoperani kuwa mwankutenda vibaya, wakúja kuwona meema amutenda, na Mwenyezimungu paaja kulamula mulumwengu-mu, iye wantukuza.

*Kuwasikirizira wenye mamulaka*

<sup>13</sup> Kwa ajili ya Mola, wasikirizeni piya wenye mamulaka wa mulumwengu-mu, Nkulu wa wafalume <sup>14</sup> na wafalume watoto, kawapéreka iye kuwahukumu wabaya na kuwasifu wenye kutenda meema. <sup>15</sup> Kamana javi ndi vyavimwajibu Mwenyezimungu, kuwa vitendo vyenu vyema-vyema viwanyamaza wajinga sawejiwa cawamba. <sup>16</sup> Inshini nkati ya uhuru wenu. Fala musitumire uhuru-wo kufisa ubaya, ila inshini kamba watumisi wa Mwenyezimungu. <sup>17</sup> Wainshimuni wanu piya, wapendeni wanduzenu wenye kwamini, mopeni Mwenyezimungu, na mwinshimuni nfalume nkulu.

*Nfano wa tabu za Almasihi*

<sup>18</sup> Umwe watumisi, wasikirizeni mamwenye wenu kwa inshima pakulu, sairi ware wenye imani waténda meema basi, fala na wagumu newo novyo. <sup>19</sup> Mwenyezimungu akusifuni ikiwa muhitamili kutabishiwa sakujuzi, konta mutabika kwa sababu ya kifulata njira ya Mwenyezimungu. <sup>20</sup> Mukihitamili pamuhukumiwa kwa sababu ya kutenda dambi, faidani? Fala mukitabika kwa sababu ya kutenda meema na kuhitamili, Mwenyezimungu akusifuni. <sup>21</sup> Kamana eco ndi camwitiriwe, konta Almasihi katabika kwa kukupendeleyani umwe, kakupani nfano ipate mufulate njira zake. <sup>22</sup> “Iye aakorire dambi anta mmoja, wala nkanywa mwake aulawire ulongo.”

<sup>23</sup> Pawakintukana, aawajibire na matukano. Paakitabishiwa, aantishire munu, ila akiripereka ka Mwenyezimungu, mwenyé kulamula shariya. <sup>24</sup> Insa iye mwaneyewe kahitamili dambi zetu mmwiri mwake pansalaba, ipate tifwire dambi, tiinshi tiwe makamilifu. Julu ya vijaraa vyake, mupata kupona. <sup>25</sup> Mida mukenendanga kamba makondoo wakwasika, fala sambu muludira ka Nsunga wenu, mwenyé kusunga roho zenu.

### 3

*Manunu na mamwenye*

<sup>1</sup> Kwa namuna mmoja, umwe manunu, kila mmoja antwii nlumake, anta awe saasikiriza Habari Ngema. Ndimana, aisakikana umwe kwamba kinu, ila kwa namuna yenu ya kuinshi iwatenze kutumaini, <sup>2</sup> pawakuwonani mukitenda vitendo vya uswafi na vya inshima. <sup>3</sup> Musishugulikire wema wa panja, kwa nfano: kusamula nywiri sana-sana, au kuvala vifure vya oru au nguwo ngema-ngema. <sup>4</sup> Kwasa javyo, wema wenu ulawe mmyoyo yenu, usiwoneke panja. Ewo wema-wo aulainika, ulawirira mmyoyo ya kurinyenyekeya na kupumuzika, ewu ndi wema uri na faida pakulu mbere ya Mwenyezimungu. <sup>5</sup> Kamana mida manunu watakatifu wakintumáini Mwenyezimungu wema-wo wakiriwaiza, julu ya kukubali mamulaka a walume wawo. <sup>6</sup> Kamba kwa nfano, Sara akintwii nlumake Iburahima, akimwita mwenye. Umwe muwa wanawe wakati wamutenda meema, samopa kinu ciwa conse cakofya.

<sup>7</sup> Na umwe mamwenye ndi novyo. Kila mmoja antafiti nkawake kwa namuna ngema. Ingawa iye kaveya koliko uwe nlume-we, mwinshimu, konta iye kapewa novyo mainsha mapya na Mwenyezimungu. Tendani javyo ipate duwa yenu musiziwiye.

*Kuinshi nfano wa Almasihi*

<sup>8</sup> Mwinsho, piya-mwe muwaze kinu kimoja noco, muwonerane utungu, mupendane, muwe na amo, na munyenyekeyane nkati ya mawazo enu. <sup>9</sup> Musiripirirane mabaya ka mabaya, wala matukano ka matukano. Kwasa javyo, wabarikini, kamana eco ndi camwitiriwe, ipate mubarikiwe. <sup>10</sup> Kamana:

“Asáka kuwa na mainsha meema  
na kummwera suku ngema,  
aziwiye lulimi rake risisowere caputu,  
wala kanywa yake isisowere ulongo.

<sup>11</sup> Basi, arisapuse mabaya, atende meema,  
akenekeze kwa nguvu zake piya ainshi salama na wenziwe.

<sup>12</sup> Kamana maso a Mola awasunga wanu makamilifu,  
masikiro ake awa wanzu kusikiriza cawalebela.  
Fala uso wa Mola ubishana na wenye kutenda ubaya.”

<sup>13</sup> Sambu, mukisakula kwa juhudi kutenda meema, nani akukutendani ubaya? <sup>14</sup> Fala anta paiwa mwankutabika kwa sababu ya kutenda meema, mujanliiwa. Basi, musiwope wala musikafilike. <sup>15</sup> Kwasa javyo, mmyoyo mwenu nturuni kuwa takatifu Almasihi, Mwenye wenu. Na akiwapo munu wakukudairini kuhusu sababu yamuri nawo tamaa, daima muwe tayari kunjibu. <sup>16</sup> Fala njibuni kwa namuna ya kurinyenyekeya na inshima, na myoyo yenu isikose mbere ya Mwenyezimungu. Basi, ikiwa wanu wankukusowererani mabaya kuhusu vitendo vyema vyamutenda kwa sababu ya umoja wenu na Almasihi, ewo wáwona haya. <sup>17</sup> Kamana vyema kutabika kwa sababu ya kutenda meema (ikiwa nafsi ya Mwenyezimungu) koliko kutabika kwa sababu ya kutenda mabaya.

<sup>18</sup> Kamana Almasihi katabika novyo paafwire kwa sababu ya dambi zenu, mara moja noyo tu basi kwa daima. Iye kamilifu, fala kafwa kwa ajili ya ware sawari makamilifu ipate akulongozeni ka Mwenyezimungu. Iye kaulaiwa mwiri wake fala kafufuriwa julu ya Roho Takatifu. <sup>19</sup> Basi, iye akilawa, akipita akereza roho zifungiwe, <sup>20</sup> ware wákiwa wabishi mida, enzi za Nnu. Mwenyezimungu akiwarinda na imani iri Nnu kankulunda safina. Nsafina-mo, wanu nane tu basi ndi wávushiwe pesire kupita mwanalukaya wakofya ire. <sup>21</sup> Ewo ndi nfano namuna vyaakuvushani Mwenyezimungu. Epa muvushiwa julu ya kufufuriwa ka Insa Almasihi, na koza ndi alama ya kutubiya kwenu. Ire ozíwe aalavire naka mmwiri mwake, ila katenda alama yakuwa na fahamu swafi mbere ya Mwenyezimungu. <sup>22</sup> Epa sambu, Insa Almasihi kakwera binguni, kawa upande wa nkono nriro wa Mwenyezimungu\*. Noko malaika, wenye mamulaka, pamoja na wenye nguvu iye wajuzi wantwii.

## 4

### *Kupinduriwa ka mainsha*

<sup>1</sup> Sambu, kwa kuwa Almasihi kâtabika mwiri wake, nomwe novyo ririmbiseni mawazo mamoja nowo. Kamana atabika mulumwengu-mu kwa sababu ya kunfulata Insa, kamariza dambi zake. <sup>2</sup> Kwa javyo, wakati umbákire mulumwengu-mu, iye ainshi akifulata vitendo vibaya vya kibinadamu, ila átenda vyavimwajibu Mwenyezimungu. <sup>3</sup> Mida wakati mwingi mukipitanga mokitenda kamba vyawatendanga wanu sawamwi-jiwa Mwenyezimungu: mutenda vitendo vya lukware, mufulata wájibu mbaya, murya na munywa, pakulu mmajambo mabaya, na mutukuza milungu ya ulongo, kitendo cakofya. <sup>4</sup> Ewo washanga pakulu futi konta sambu amufulata vitendo vibaya vyawatenda ewo, na wakitukanani. <sup>5</sup> Fala ewo wájuzi wajibu ka Mwenyezimungu, ire óka kuwalamula wanu piya, wafwire na wari hai. <sup>6</sup> Kwa sababu ya javyo, Habari Ngema wereziwa anta na wafwi, ipate wainshi nroho zawo (kamba vyaari Mwenyezimungu), ingawa mwiri wawo upokerera hukumu yakufwa yawatabika wanu piya.

<sup>7</sup> Mwinsho wa vinu piya uwa karibu. Ndimana, mujuzi muridume wanyewe na murinang'anizire, ipate mulebele duwa. <sup>8</sup> Visitoshe, zidini kupendana, konta pendo rifuta dambi nyingi. <sup>9</sup> Mupane malazi bila kudugudana. <sup>10</sup> Kamba kila mmoja vyaapokerere uwezo maalumu, atumire sana-sana kuwatumika wenziwe, awe ntumisi mwema wa uwezo jisijisi wa Mwenyezimungu. <sup>11</sup> Asowéra, asowere usemi waapewa kwereza

\* 3:22 “Nkono nriro wa Mwenyezimungu” ndi mahala bora pakulu.

na Mwenyezimungu. Javyo, kwa piya hali, Mwenyezimungu atukuziwe, julu ya Insa Almasihi. Utukufu na uwezo ndi wake iye daima milele. Aamina.

*Kutabika kwa sababu ya kunfulata Insa*

<sup>12</sup> Wapendani wangu, paakulawirirani mambo magumu a kuyererwa, musikafilike kamba cukukunireni kinu cakutajabisa. <sup>13</sup> Kwasa javyo, kwa kuwa mwankutabika kuntabikira Almasihi, muwe radi, ipate novyo pausaka kufafanuriwa utukufu wake mulumwengu-mu, umwe novyo mufurahi ka radi pakulu. <sup>14</sup> Ikiwa mutukaniwa kwa sababu ya kunfulata Almasihi, mujanliiwe konta Roho wa utukufu na wa Mwenyezimungu apumula julu yenu. <sup>15</sup> Fala ikiwa mwankutabika, isiwe kwa sababu ya kuulaya, kwiwa, kutenda ubaya, au kwa kushugulikira mainsha a wanu wengine, <sup>16</sup> ila ikiwa mwankutabika kwa sababu ya kunfulata Insa, aipo aibu. Kwasa javyo, ntukuzeni Mwenyezimungu, kwa kuwa mukwijiwikana kwa zina rake. <sup>17</sup> Konta wakati wakulamuriwa wanu uwa karibu, na waja kuwa watanzi kulamuriwa ndi wana\* wa Mwenyezimungu. Na ikiwa ofwe wafulati wa Insa tilamuriwa, sambi ware sawakubali Habari Ngema ya Mwenyezimungu, mwinsho wawo ndi wepi? <sup>18</sup> Na,

“Ikiwa makamilifu virigariga kuvushiwa, sambi wabaya na wamadambi, cija kuwakuna kinani?”

<sup>19</sup> Basi, ware wari kutabika kwa sababu ya kufulata vimwajibu Mwenyezimungu, waripereke mmakono mwa Mwenyezimungu mwenye kauli awombire, kuno wakizidi kutenda meema.

5

*Ngano ka walongozi na wanemba njamati*

<sup>1</sup> Sambu, omi novyo niwa nlongozi wa jamati kamba umwe, niwa shahidi wakutabika ka Almasihi, na nukuwa upande wa utukufu pausaka kufafanuriwa. Kwa javyo, nkati yenu umwe walongozi nukutafadilini javi: <sup>2</sup> Sungani nfuwo wa Mwenyezimungu\* uri kati yenu, sairi kwa kuwalazimisha ila ka moyo radi kamba vyaasaka Mwenyezimungu, sairi kwa anzima yakupata faida ila kwa anzima yakweli yakuwasaidiya wanu wengine <sup>3</sup> Musiwalongoze wanu wamugabiziwe kwa namuna ngumu, ila muwe mifano myema kwa wanu wenu wakusungani. <sup>4</sup> Basi, akifika Nkulu wa wasunga, Insa Almasihi, mupokerera lemba ra utukufu, sarisa tena kung'anira kwake. <sup>5</sup> Kwa namuna mmoja noyo, umwe wanemba, kubalini mamulaka a walongozi wenu. Piya muvare unyenyekevu, konta Mandiko akwamba javi:

“Mwenyezimungu abishana na wanu wakuridai, fala awarehemu wanu wakurinyenyekeya.”

<sup>6</sup> Basi rinyenyekeyeni mbere ya uwezo nkulu wa Mwenyezimungu, ipate ka wakati wake maalumu waaturire, aje akusifuni. <sup>7</sup> Ngabizini tafauti zenu, konta akusungani. <sup>8</sup> Muwe tayari na murinang'anizire konta aduwi wenu, Ibilisi, kawankukulumbatani nanyenje kamba simba vyaturuma, akisakula kunkola munu ankapire. <sup>9</sup> Ririmbiseni kubishana naye, moloke na kwamini kwenu, kwa kuwa mukwijiwa kuwa wafulati wengine watawanyike mulumwengu-mu wawankutabika kamba vyamuri kutabika umwe. <sup>10</sup> Na bandi ya kutabika wakati aba, Nlungu mwenye rehema piya, waakwitani muwe upande wake wa utukufu wa milele julu ya kulungana kwenu na Almasihi, akukamilishani, akwakikishani, akupani nguvu na akutengemanisani. <sup>11</sup> Iye ndi mwenye uwezo piya daima milele! Aamina.

*Salamu za mwinsho*

<sup>12</sup> Sila†, nduyetu wanintula kuwa na kauli, kankunisaidiya kukwandikirani eyi waraka noto javi-yi. Nisaka nukurimbiseni myoyo yenu na nukwakikisheni kuwa eyi ndi rehema yakweli ya Mwenyezimungu. Noyi rehema-yi ikoloseni! <sup>13</sup> Wenye kwamini Babiloniya‡,

\* 4:17 Kigeregu: “jamaa”. \* 5:2 Mana ake: wanu wa Mwenyezimungu. † 5:12 Sila zina rengine Silvanu.

‡ 5:13 “Babiloniya” mana ake Roma, au kaya nyengine wenye kwamini wakiinshi kiyeni.

watondoriwe pamoja nomwe, wakuperekerani salamu. Maruku, mwanangu julu ya kwamini, iye novyo akuperekerani salamu. <sup>14</sup>Mukomazane kwa alama yakolota pendo<sup>§</sup>. Salama iwe pamoja namwe piya mulungane na Almasihi.

---

<sup>§</sup> 5:14 Alama ya kolota pendo nkiyahudi ndi “beju”.

## Waraka 2 ya Peduru

### Mwanzo

Peduru kandika eyi waraka-yi nkalaboshu mmojawapo ya Roma, kiyasi ca myaka wa 67-68 bandi ya Almasihi, wakati aba kábula ya kuka kuulaiwa. Akikaidi kufunda sakuna deretu kawakifunda wanu wengine (sura ya 2). Akwamba kuwa Injili ndi kinu catikijuzi kwamini kwa kutumaini.

Sura ya 3, Peduru asowera kuhusu ukweli wa kuludi ka Insa na kulamuriwa ka mwinsho. Kwa sababu ya noci tikijuzi tiinshi wakati watirindira kuvushiwa kaawapere tamaa wenye kwamini.

### *Salamu*

<sup>1</sup> Omi Ansumani Peduru, ntumisi na walii wa Insa Almasihi, eyi waraka-yi niwaperekera piya wapatire kwamini ka faida pakulu kamba ofwe vyataminire. Kwamini-ko tipata julu ya ukamilifu wa Nlungu wetu, Nvushi Insa Almasihi.

<sup>2</sup> Rehema na salama mongeziwe, julu ya kumwijiwa Mwenyezimungu pamoja na Insa, Mwenye wetu.

### *Kwitiwa ka wenye kwamini*

<sup>3</sup> Kwa uwezo waari nawo iye kwa kuwa ndi Nlungu, iye katipa piya vyatisakula ipate tiinshi mainsha akumwajibu Mwenyezimungu. Tipata julu ya kumwijiwa ire atítire kupokerera utukufu wake pamoja na wema wake mwaneyewe. <sup>4</sup> Kwa namuna-yi, Mwenyezimungu katipa tamaa ya faida pakulu na ya matajabisa, ipate julu yawo mulawirire kuwa na namuna za Mwenyezimungu, kuwa mupolonyosiwa uwaribifu wa mulumwengu-mu, ushongiwa julu ya wájibu wa dambi. <sup>5</sup> Ndimana, tumirani nguvu zenu piya musanganye kwamini na wema, wema na wijiwifu, <sup>6</sup> wijiwifu na kurimiliki, kurimiliki na kuhitamili; kuhitamili na namuna ya kumwajibu Mwenyezimungu, <sup>7</sup> namuna ya kumwajibu Mwenyezimungu na kupendana, na kupendana musanganye na kuwapenda wanu piya. <sup>8</sup> Kamana namuna-zi, mukiwa nawo nezo zikizidi kukula kati ya mainsha enu, zukutenzani kuwa wijiwifu wenu wa kumwijiwa Mwenye Insa Almasihi auwepo bila visumo ila kukuja na faida. <sup>9</sup> Kamana ware sawatenda vitendo vya faida-vyo, ewo awawona, uwengira mwiza, wariwala kuwa Mwenyezimungu mida kâwaswafi madambi awo.

<sup>10</sup> Ndimana wanduzangu, tumirani nguvu zenu piya mwakikishe kuwa kweli-kwelini mwitiwa na mutondoriwa na Mwenyezimungu. Mukitenda javyo, amushubutu kwasa kwamini kwenu. <sup>11</sup> Kamana kwa namuna-yo, uwapo nryango nkulu wakufunguririwa sana ipate mwingire muufalume wa milele wa Insa Almasihi, Mwenye wetu na Nvushi wetu.

### *Kutunza Mandiko Matakatifu*

<sup>12</sup> Kwa javyo, niya yangu ndi kukukumbusani evi vinu-vi daima, ingawa mukwijiwa futi na mukwakikishiwa nkati ya ukweli wamupokerere. <sup>13</sup> Níwaza kuwa níjuzi nukukumbuseni, wakati waniripo mulumwengu-mu, <sup>14</sup> konta, kamba vyaanolotere Mwenye wetu Insa Almasihi, nukwijiwa kuwa suku karibu eya mainsha-ya nukwasa. <sup>15</sup> Na nítenda juhudi piya ipate, bandi yakulawa omi mulumwengu-mu, daima evi vinu-vi mukumbukire.

### *Ushahidi wakolota kuwa Habari Ngema yakweli*

<sup>16</sup> Kamana patikerezanga uwezo wa Mwenye wetu, Insa Almasihi, na kuludi kwake, sikuwa tikifulata hadisi ya ujanja, ila tereza ubora wake nkulu kwa kuwa tîwona na maso etu wanyewe. <sup>17</sup> Kamana iye paapokerere swifa na utukufu ka Mwenyezimungu Baba wake, ofwe tikiwapo. Paasikire shauti ya utukufu pakulu ya Mwenyezimungu ikamba: “Eyu ndi Mwanangu wanimpenda pakulu.



Niwa radi naye pakulu”,

<sup>18</sup> ofwe wanyewe tisikira eyo shauti-yo kulawa mbinguni. Tisikira kamana pamwango takatifu, tikiwa onse na Insa.

<sup>19</sup> Visitoshe, tanawo uhakika pakulu kwa sababu ya habari zereziwe na minabii. Habari-zo vyema mutengemane konta ndi kamba nuru vyaimwarika pamahala pakwinukala. Ikusaidiyani mpaka suku yakuja Almasihi, na nuru yake ikuja kumwarika ngwê mmyoyo mwenu kamba ng'andu. <sup>20</sup> Kinu bora pakulu, ijiwani kuwa piya vibushuriwe mMandiko avilawire nkiswa mwa nabii mmojawapo. <sup>21</sup> Kamana avipo vibushuriwe kwa nafsi ya binadamu, ila Roho Takatifu ndi awalongoze wanadamu kusowera usemi ulawire ka Mwenyezimungu.

## 2

### *Wanlimu walongo*

<sup>1</sup> Fala mida-po, wâkiwapo minabii walongo nkati ya wanu, kamba vyawaja kulawirira wanlimu walongo kati yenu umwe. Ewo wakuja nawo kisiiri-siiri inlimu zakufuja, mpaka wankatala Mwenye kuwombola. Kwa javyo, waritisira upesi kwaribiwa. <sup>2</sup> Wanu wengi wakuja kufulata namuna zawo za lukware, na kwa sababu zawo, wanu wakuja kusowerera caputu njira yakweli. <sup>3</sup> Ewo wanlimu walongo-wo, kwa kuwa wasaka wapate nzuruku mwingi, wakuja wapate faida kwa usowezi wa ulongo. Fala tangu mida hukumu yawo ilamuriwa, na Mwenyezimungu kawa tayari kuwapoteza.

<sup>4</sup> Kamana malaika pawakorire dambi, Mwenyezimungu aawasire kupolonyoka, ila kawapereka motoni, akiwasa wafungiwe ngiza mpaka suku ya Kiyama. <sup>5</sup> Novyo, aawasire kupolonyoka wanu wa mida paawaperekere mwanalukaya sawamopa Mwenyezimungu mulumwengu-mu. (Ndi kweli kanvusha Nnu, mwenyé kuweréza wanu njira ya shariya, pamoja na wanu saba). <sup>6</sup> Na kahukumu novyo makaya makulu a Sodom na Gomora. Katadusa rivu na kalamula hukumu\*. Kolota kaya-zo ziwe nfano wa namuna vyaaja kuwatenda piya wanu ware sawamopa. <sup>7</sup> Upande mwengine, Mwenyezimungu kanvusha Loti, mwenyé shariya, katabika kwa sababu ya vitendo vya ucaputu vya wanu wabaya. <sup>8</sup> (Kamana Loti âkiwa munu wa shariya, fala kila suku kazunguriziwa na wabaya. Iye kâkafilika pakulu kwa sababu ya vitendo vibaya vyaakisikira na vyaakiwona.) <sup>9</sup> Basi, ndi kweli kuwa Mola akwijiwa namuna yakuwavusha nkati ya kuyereririwa ware wamwinshimu, na yakuwaturira hukumu sawana shariya suku ya Kiyama. <sup>10</sup> Kuzidi pakulu, akuja kuwahukumu ware wafulata wâjibu wawo wa ubaya wa kibinadamu, na wakejeli mamulaka.

Nowo wanlimu wa ulongo-wo waridâi na waritenza. Awawenshimu viyumbe vya utukufu mbinguni, ila wakufuru. <sup>11</sup> Anta malaika, nowo wari na nguvu pakulu na uwezo kuwapunda nowo, awasowera mbere ya Mwenye, usemi wacaputu wakubishana na novyo viyumbe-vyo. <sup>12</sup> Fala ewo wawa kamba wadudu sawawaza kinu, wafulata wâjibu wawo wa kibinadamu. Wainshi ipate wakoriwe na waulaiwe. Wakufuru kuhusu mwaha wawatikina. Basi, kwa namuna vyawaja kupoteziwa wadudu-wo, newo novyo wakuja kupoteziwa kwa uwaribifu wawo wanyewe. <sup>13</sup> Ewo watabika na ubaya ndi nshahara wa ubaya wawo. Viwajibu kufulata wâjibu wawo mbaya nsana juwa rikiwala. Ewo noda na vilaso†, viwajibu kukutesani‡ kumbe wakuja mmajambo enu a sherehe. <sup>14</sup> Mmaso mwawo uwejala uzinzi na awatosheka kukola dambi. Viwajibu kuwatesa na kuwakoresa wanu sawakamilike, myoyo yawo izowerera wâjibu wa vinu. Ewo wanu-wo walaniwa! <sup>15</sup> Wasapuka njira ngema, wasika. Wafulata njira ya mwananlume wakwitiwa Balamu§, mwana wa Bewori, kumwajibire kupata nzuruku kwa vitendo vibaya. <sup>16</sup> Balamu kasutumiwa kwa dambi yake mwananyewe. Buru saanasowera, kâsowera na shauti kamba munu, na uzozo wa nabii-yo uziwiwa.

\* 2:6 “Kalamula hukumu” kuwa isiludire kujengiwa tena upya. † 2:13 Ona 3:14. ‡ 2:13 Ona 12. § 2:15 Ona Isabu 22:21-35.

<sup>17</sup> Wanlimu walongo-wo wawa kamba nrimbu sauna maji, au kamba mawingu akiveverusiriwa baidi na mepo\*. Ewo Mwenyezimungu kawaturira mamburo awo pagiza, pakwinukala pí†. <sup>18</sup> Kamana warisifu wanyewe na masemo seleweka. Watumira wájibu mbaya wa kibinadamu ipate wawatase wawakorese ware wakuwa kwa suku aba wâwatira ware waínshi vibaya. <sup>19</sup> Wawapa tamaa ya uhuru, filihali ewo wanyewe watwana wa tabiya zakudangula. Kamana kinu ciri kunkidiri munu, iye ntwana wa noco kinu-co. <sup>20</sup> Kamana ndi javi: munu, julu ya kumwijiwa Insa Almasihi, Mwenye wetu na Nvushi wetu, anusurika na vibaya mulumwengu-mu. Fala ikiwa aringiza tena upya novyo vitendo vibaya-vyo, vikinkidiri, mainsha ake akuwa caputu pakulu kupunda pakwanza. <sup>21</sup> Fadari munu-yo anatowa kwijiwa njira ya ukamilifu, koliko kwijiwa ikisa kukatala ámuri takatifu yaapewe. <sup>22</sup> Munu kamba eyu atimiza usowezi wakweli wamba javi: “Umbwa kaludira kurya matapisi ake mwaneyewe.” Na atimiza novyo usowezi mwengine wamba: “Nguluwe wakoziwa kaludira kurinyaula ntopetope.”

## 3

*Kuludi ka Mwenye Insa*

<sup>1</sup> Wapendani wangu, eyi ndi waraka yapiri yanukwandikirani. Wo-wawiri, nisakula nukulamuseni ankili zenu ngema mukumbukire, <sup>2</sup> ipate mukumbukire vyawambire mida minabii takatifu, na ámuri za Mwenye wetu, Nvushi, zaalazimishe julu ya mawalii wenu.

<sup>3</sup> Kinu bora pakulu, mwijiwe kuwa, suku za mwinsho, wakuja kulawirira wanu wamojawapo wakufezeyi ukweli, wafulata piya wájibu wawo wa dambi. <sup>4</sup> Wakwamba javi: “Insa kakupani tamaa kuwa aludi, nikamba? Sambi, kawa ndepi? Tangu wakati wa babu zetu, mwanzo wa duniya, vinu vingari vikenenda namuna moja noyo!” <sup>5</sup> Ewo wanuwiya kukatala kuwa tangu mida Mwenyezimungu komba bingu, na kwa ámuri yake, iye kawanya duniya na maji, katula ardhi yakumiliya julu ya maji. <sup>6</sup> Ikisa maji-yo iye katumira kudangula ulumwengu kwa kumpereka mwanalukaya nkulu. <sup>7</sup> Fala julu ya ámuri moja noyo, bingu na ardhi virípo sambi-pa vituriwa, ipate viteketeziwe na moto wa suku ya Kiyama. Wakati-wo wanu wabaya wakuka kwaribiwa nfululu.

<sup>8</sup> Fala wapendani wangu, musiriware kuwa mbere ya Mwenye, suku moja ndi kamba myaka alufu, na myaka alufu ndi kamba suku moja. <sup>9</sup> Kusema kweli, Mwenye aakawa kutimiza tamaa zake kamba vyawawaza wanu wengine. Anta, iye akoloterani imani yake, avimwajibu kuwa munu mmojawapo apoteye, ila asaka kuwa wanu piya watubiye. <sup>10</sup> Fala suku yakuja Mwenye alawirira kamba mwivi. Suku-yo kukuja kudidima pakulu futi, bingu ilainika, na mwezi\* piya vikociwa, vilainika. Ardhi pamoja na vitendo vikúna muardhi, piya viwoneka†.

<sup>11</sup> Kwa kuwa vinu piya vikuja kupoteziwa javyo, ndi bora pakulu kuinshi namuna takatifu vyaakumwajibu Mwenyezimungu, sinovyo? <sup>12</sup> Noyo suku ya Mwenyezimungu-yo, murindire na radi, tendani juhudi ifike upesi. Kwa sababu ya kuja ka noyo suku-yo, bingu ikorera ifujika, na mwezi piya vikuja kociwa visuluka. <sup>13</sup> Fala kamba Mwenyezimungu vyaatipere tamaa, tírindira bingu nyipya na ardhi nyipya, mahala mwakutendiwa vinu piya kwa shariya.

<sup>14</sup> Basi wapendani wangu, kwa kuwa evi vinu-vi murindira, rimbani kwa nguvu zenu piya ipate iye akusinganeni muwe na salama naye, bila noda wala kilaso. <sup>15</sup> Na imani ya Mwenye wetu, tulani kamba nafasi yakupata kuvushiwa. Kinu-ci sawa-sawa na vire nduyetu, mpendani wetu Paulu, kwa kufulata wijiwifu waapewe, vyaakwandikireni. <sup>16</sup> Piya waraka zaandike kuhusu ewu mwaha-wu, zisema kinu kimoja. Ndi kweli kuwa muwaraka-zo, viwapo vinu vimojawapo vyakurigariga kwelewa. Watikínifu na wanu sawakamilike, vinu-vyo wazungunusa wakwereriwa caputu ipate waripoteze, kamba vyawatenda novyo aya nyengine mMandiko Matakatifu.

\* 2:17 Awatenda kamba vyawajuzi kutenda. Ona Yuda 12. † 2:17 Ona Yuda 13. \* 3:10 Au: “vinu”. † 3:10 Au: “vikolotiwa ipate vilamuriwe”.

<sup>17</sup> Ndimana, umwe wapedani wangu, kwa kuwa evyo vinu-vyo mwijiwa futi, ri-nang'anizireni ipate musitesiwe kwa makosa a wanu sapana shariya, kwasa koloka kwenu. <sup>18</sup> Fala zidini kukula nkati ya rehema na wijiwifu wa Insa Almasihi, Mwenye wetu na Nvushi wetu.

Iye apewe utukufu, sambi-pa na kwa milele. Aamina.

## Waraka 1 ya Yahaya

### Mwanzo

Eyi waraka-yi yandikiwa na Yahaya walii. Yahaya ákiwa mwenziwe pakulu Mwenye Insa wa pamoyo pake. Wandikiriwa wenye kunfulata Insa, na ikwereza sana-sana kuwa kweli-kwelini Mwenyezimungu karitenda kuwa mwanadamu julu ya Insa Almasihi. Eku kufunda-ku kukisakikana konta wengine wakifunda kuwa Insa siyo kweli-kwelini mwanadamu na siyo nlungu wa kweli.

Yahaya awona kuwa wenye kwamini wa kweli wafulata inlimu ya kweli, wafulata kufunda kajavi na kupendana munu na mwenziwe.

Yahaya kandika eyi waraka-yi kaya itíwa rero Turkiya, mwinsho wa sekulu ya kwanza bandi ya Almasihi.

### *Nsemi wa mainsha*

<sup>1</sup> Tukwerezani kuhusu Nsemi wa mainsha, ákiwapo tangu mwanzo. Tînsíkira, tîmmona na maso etu, tînshuhudiya, na tînkola na makono etu. <sup>2</sup> Noyo mainsha-yo olótiwa. Timmona, ntamana tilavya ushahidi, tukwerezani kuwa iye ndi Mwenyé mainsha wa milele, ákiwa na Baba na toloteriwa ofwe. <sup>3</sup> Vyatîmmonire na vyatînsikire, tukukwerezani umwe novyo ipate nomwe muwe na ujamaa nafwe. Ujamaa wetu uwa na Baba pamoja na Insa Almasihi, Mwanawe. <sup>4</sup> Na ezi habari-zi tukwandikirani ipate radi yetu\* itimiziwe.

### *Enenda nnuru*

<sup>5</sup> Sambi, eyi ndi habari yatinsikire iye na tukwerezani umwe, kuwa Mwenyezimungu ndi nuru. Nkati yake kisi anta aba acishubutu kuwepo. <sup>6</sup> Tikámba kuwa tanawo umoja naye kuno tikenenda pakisi, tilongopa, atíténda ukweli. <sup>7</sup> Fala ikiwa tikwenenda panuru, kamba iye vyaari panuru, tikuwa nawo umoja watupu, na damu ya Insa Mwanawe ítiswafi madambi piya.

<sup>8</sup> Tikámba kuwa atina dambi, tankuritesa, ukweli aupo nkati yetu. <sup>9</sup> Fala ikiwa tikweréza dambi zetu, iye mwaminifu na mwenyé shariya, átiswamii madambi etu, na átiswafi nkati ya vitendo vibaya piya. <sup>10</sup> Fala tikámba kuwa atinakola dambi, sawa-sawa na kwamba iye nlongo, usemi wake aupo mmoyo mwetu.

## 2

<sup>1</sup> Wasimana wangu, ezi habari-zi nukwandikirani ipate musikore dambi. Fala ikiwa munu mmojawapo akola dambi, tanawo wakutímírira mbere ya Baba, Insa Almasihi, Nkamilifu. <sup>2</sup> Iye ndi kafara iripa kwa madambi etu, na siyo kafara kwa madambi etu basi, fala kwa madambi a wanu wa mulumwengu-mu piya.

<sup>3</sup> Na alama itolótera kuwa timwijíwa iye ndi kuwa tifulata ámuri zake. <sup>4</sup> Munu akamba: “Nímwijíwa” fala safulata ámuri zake, munu-yo nlongo, ukweli aupo mmoyo mwake. <sup>5</sup> Fala afuláta usemi wake, nkati yake pendo ra Mwenyezimungu riwankukamilika kweli-kwelini. Kitendo colóta kuwa tilungana naye ndici: <sup>6</sup> mwenyé kwamba kuwa alungana naye, inlazimu enende kamba vyenende Insa mulumwengu-mu.

### *Ámuri nyipya*

<sup>7</sup> Wapendani wangu, ámuri yanukwandikirani-yi siyo nyipya, fala ámuri ya mida, ya tangu mwanzo. Eyi ámuri ya mida ndi habari yamusikire. <sup>8</sup> Novyo-sivyo, vyanukwandikiri-rani-vi ámuri nyipya, vyauri ukweli kwake iye na kwenu umwe, konta kisi caankwisa, nuru yakweli ilangaza futi.

\* 1:4 Au: “yenu”.

<sup>9</sup> Munu amba: “Nankwenenda na nuru”, iri amwina nduye, narero kankwenenda nkisi.  
<sup>10</sup> Ampénda nduye akuwa nnuru, na mmoyo mwake aciwepo cakunkwakurisa. <sup>11</sup> Fala ire amwína nduye abaki nkisi, kankwenenda nkisi, eejiwa kooka konta kisi cimwinúkaza kumaso.

<sup>12</sup> Umwe wasimana wangu, nukwandikirani  
 konta kwa zina rake muswamiiwa madambi enu.

<sup>13</sup> Umwe wawáwa, nukwandikirani  
 konta mumwijiwa ire akiwapo tangu mwanzo.

Nukwandikirani umwe, wanemba,  
 konta munshinda Ibilisi\*.

<sup>14</sup> Umwe wasimana wangu,  
 nukwandikirani konta mumwijiwa Baba.

Umwe wawáwa, nukwandikirani,  
 konta mumwijiwa ire akiwepo tangu mwanzo.

Umwe wanemba, nukwandikirani konta mukomala,  
 usemi wa Mwenyezimungu ubaki mmyoyo mwenu,  
 na munshinda Mbaya†.

#### *Usukwajibuni ulumwengu*

<sup>15</sup> Usukwajibuni ulumwengu wala virípo mulumwengu. Íkiwa munu mmojawapo umwajibu ulumwengu, eyo munu-yo aampenda Baba. <sup>16</sup> Konta piya virípo mulumwengu-mu, vinú-vi: wájibu wa kimwiri, wájibu wa maso mawoni, na maritenzi a vinu vya mulumwengu-mu, avilawa ka Baba, vilawa mulumwengu nómu. <sup>17</sup> Ewu ulumwengu-wu pamoja na vitendo vyake vibaya vyakwajibisa, piya vípita. Fala ire aténda nafsi ya Mwenyezimungu áinshi milele.

#### *Musitesiwe*

<sup>18</sup> Umwe wasimana, ezi suku za mwinsho. Kamba vyamusikire kuwa akúja aduwi wa Almasihi, sambi wankulawirira maaduwi wa Almasihi wengi wawenye. Ndimana tukwijiwa kuwa ndi suku za mwinsho. <sup>19</sup> Maaduwi-wo waláwa kati yetu, fala awawere kweli-kwelini wa daraja yetu. Kamana kamba wákiwa wa daraja yetu, nanga wabaki nofwe. Falakini ewo watasa ipate vijiwikane kuwa anta mmoja awere wa daraja yetu. <sup>20</sup> Fala umwe, Ntakatifu kakumiminirani Roho Takatifu, na piya-mwe mukwijiwa ukweli. <sup>21</sup> Sukwandikirani kwa kuwa mútikina ukweli, ila nukwandikirani kwa kuwa mukwijiwa ukweli, na mukwijiwa kuwa nkati ya ukweli aupo ulongo. <sup>22</sup> Nlongo nani? Nlongo ndi ire akaídi kuwa Insa ndi Almasihi. Ire ankána Baba pamoja na Mwanawe, noyo ndi aduwi wa Almasihi. <sup>23</sup> Piya ankana Mwana onse ndi sawalungana novyo na Baba. Fala mwenyé kumwakikisha Mwana kalungana na Baba novyo.

<sup>24</sup> Habari zamusikíre tangu mwanzo, tulani mmoyo. Ikiwa umwe mutula mmoyo habari zamusikíre tangu mwanzo, mukuwa pamoja na Mwana na Baba novyo. <sup>25</sup> Na tamaa yaatipere Insa ndiyi: mainsha a milele! <sup>26</sup> Nukwandikirani ezi habari-zi kuhusu ware wasakúla kukutesani. <sup>27</sup> Fala umwe-po, Roho Takatifu waakumiminíreni Insa-yo mubaki naye daima, ndimana amusakula kufundiwa kinu kimojawapo na munu. Ila Roho Takatifu wamumiminiriwe-yo akufundani vinu piya. Na kwa kuwa kufunda-ko siko ka ulongo, ka kweli, bakini na Insa, kamba vyamufundiwe.

#### *Wana wa Mwenyezimungu*

<sup>28</sup> Sambu, umwe wasimana wangu, zidini kulungana naye, ipate paasaka kuja, isitipate aibu mbere yake, ila tiwe nawo uhakika. <sup>29</sup> Kamba vyamwijiwa kuwa iye kamilifu, mwijiwe kuwa kila mwenyé kutenda ukamilifu onse, mwana‡ wa Mwenyezimungu.

\* 2:13 Kigeregu: “Mbaya”. † 2:14 “Mbaya” mana ake Ibilisi. ‡ 2:29 Kigeregu: “kapongoriwa”.

## 3

<sup>1</sup> Ngatunzani pendo rikulu Baba raatipa ofwe, mpaka ofwe kupata kwitiwa wana wa Mwenyezimungu! Na kweli-kwelini, ofwe tiwa wanawe! Ndimana wanu mulumwengu-mu awatijiwa, konta iye awamwijiwa. <sup>2</sup> Wapendani wangu, sambu tiwa wana wa Mwenyezimungu. Catisaka kuwa acinarolota, fala tukwijiwa kuwa Insa paasaka kuja, tilandana naye, konta tímmona iye vyaari. <sup>3</sup> Na kila mwenyé kutumaini onse tamaa-yi, áriswafi, kamba iye vyaari swafi.

<sup>4</sup> Akolanga dambi onse kankutupa shariya ya Mwenyezimungu. Dambi ndi kutupa shariya mojawapo. <sup>5</sup> Mukwijiwa kuwa iye kâja atilavye dambi. Neye aana dambi. <sup>6</sup> Kila mwenyé kulungana naye aazidi kukola dambi. Kila mwenyé kuzidi kukola dambi aanamba kummona wala kumwijiwa.

<sup>7</sup> Umwe wasimana wangu, asukuteseni munu. Aténda ukamilifu ndi kamilifu, kamba iye vyaari kamilifu. <sup>8</sup> Aténda tabiya ya kukola dambi wa Ibilisi, konta Ibilisi kazi yake tangu mwanzo ndi dambi. Kwa javyo, Mwana wa Mwenyezimungu\* karolota ipate afuje vitendo vya Ibilisi. <sup>9</sup> Kila mwenyé kupongoriwa upya na Mwenyezimungu onse aatenda tabiya ya kukola dambi, konta mbeyu† yake iwa kati yake. Iye aazidi kukola dambi, konta kapongoriwa upya na Mwenyezimungu. <sup>10</sup> Kwa namuna-yi ndi patijiwa kusiyana kuripo nkati ya wana wa Mwenyezimungu na wana wa Ibilisi: saatenda ukamilifu na saampenda nduye onse, neye novyo siyo wa Mwenyezimungu.

*Uwé pamoja na Insa, mupendane*

<sup>11</sup> Habari yamusikire tangu mwanzo ndiyi: tijuzi tipendane. <sup>12</sup> Tisinlande Kaini âpatiwe na Ibilisi, akimuulaya nduye. Kâmuulaya sababuni? Konta vitendo vyake víkiwa vibaya fala vya nduye víkiwa vya ukamilifu.

<sup>13</sup> Wanduzangu, wanu sawamwijiwa Mwenyezimungu wakukwinani, musishange. <sup>14</sup> Ofwe tukwijiwa kuwa tisa kulawa nkati ya kifo, tingira nkati ya mainsha, konta tiwapenda wanduzetu. Munu saampenda nduye angari nkifo. <sup>15</sup> Mwenyé kumwina nduye ndi kisomi. Mukwijiwa kuwa aapo kisomi anta mmoja wakuwa nawo mainsha a milele. <sup>16</sup> Javyo ndi patijiwa mana a pendo: Insa Almasihi kapereka mainsha ake kwa ajili yetu. Ndimana nofwe novyo tíjuzi tipereke mainsha etu kwa ajili ya wanduzetu. <sup>17</sup> Fala ikiwa munu kanawo mali, na kankummona nduye cintowa kinu, fala anfungira wajii, pendo ra Mwenyezimungu akuwa nawo mwaja? <sup>18</sup> Basi, wasimana wangu, tisimpende munu na masemo a nkanywa tu basi, ila timpende kwa vitendo na ukweli. <sup>19</sup> Javyo ndi patijiwa kuwa tiwa wanu wa kweli, na mbere ya Mwenyezimungu myoyo yetu itengemana. <sup>20</sup> Kamana myoyo paitilaumu ponse, tijiwe kuwa Mwenyezimungu ndi nkulu zaida ya myoyo, iye akwijiwa vinu piya.

<sup>21</sup> Wapendani wangu, íkiwa myoyo yetu aitilaumu, tanawo uhakika mbere ya Mwenyezimungu. <sup>22</sup> Catinlébela conse típata kwake iye, konta tifulata ámuri zake na títenda vimwajibu. <sup>23</sup> Ámuri yake yawenye ndiyi: kunkubali Mwanawe, Insa Almasihi, na kupendana kamba vyaatamúrire. <sup>24</sup> Mwenye kifulata ámuri zake, kalungana na Mwenyezimungu, na Mwenyezimungu kalungana neye. Neci ndi citijiwisa kuwa iye kalungana nofwe: julu ya Roho Takatifu waatipere.

## 4

*More-more na wanlimu walongo*

<sup>1</sup> Wapendani wangu, musiwakubali piya wamba wáfunda kwa Roho wa Mwenyezimungu, fala kwanza watunzeni nowo wanu-wo, mwijiwe kuwa wa Mwenyezimungu au siwo. Konta mulumwengu-mu wankulawirira minabii wengi walongo. <sup>2</sup> Umwe mumwijiwa Roho wa Mwenyezimungu kwa namuna-yi: piya roho zakwakikisha kuwa

\* 3:8 “Mwana wa Mwenyezimungu” ndi zina rimojawapo retiwa Insa. Rikolota kupatana kwema ka Insa na Mwenyezimungu, kamba mwana na wawaye. Eri zina-ri aisema kuwa cipita kitendo ca muka na nlume, ila kupatana kukulu ka kiroho. † 3:9 Mbeyu ndi namuna ya mainsha mapya.

Insa Almasihi kaja kibinadamu, wanu-wo wa Mwenyezimungu. <sup>3</sup> Fala piya roho za wanu zinkána Insa, wanu-wo siwo wa Mwenyezimungu. Roho zawo za uaduwi ka Almasihi. Kamba vyamusikire kuwa roho ya aduwi-yo ikúja kulawirira, nepa iwapo futi mulumwengu nomu.

<sup>4</sup> Wasimana wangu, umwe muwa wa Mwenyezimungu, mwisa kuwashinda maaduwi-wo. Konta arípo nkati yenu\* ndi ari na uwezo pakulu koliko ire arípo mulumwengu-mu. <sup>5</sup> Ewo wanu wa mulumwengu-mu, ndimana wásowera mambo a mulumwengu, na wanu mulumwengu-mu wásikiriza. <sup>6</sup> Ofwe tiwa wanu wa Mwenyezimungu. Amwijíwa Mwenyezimungu onse atisikiriza, fala saari upande wa Mwenyezimungu aatisikiriza. Javyo ndi patijiwa roho ya ukweli na ya ulongo.

#### *Pendo ra Mwenyezimungu*

